

**Abdilatif Abdalla** alizaliwa Mombasa, Kenya mwaka 1946. Baada ya kuandika na kusambaza karatasi inayoitwa *Kenya: Twendapi?* alifungwa gereza kwa miaka mitatu (1969-72) Ilikuwa katika muda huo wa kufungwa kwake alipoandika diwani yake maarufu ya *Sauti ya Dhiki* (1973). Baadaye aliendelea kuandika mashairi na insha vinavyopatikana kwenye majarida na mikusanyo mbalimbali. Baada ya kutoka kifungoni alikimbilia Dar es Salaam alikofundisha Chuo Kikuu. Halafu alihamia London ambako alifanya kazi kwenye Shirika la Utangazaji la Uingereza BBC, kabla ya kwenda Ujerumani alikofundisha Kiswahili kwa miaka mingi katika Chuo Kikuu cha Leipzig.

**Euphrase Kezilahabi** alizaliwa Namagondo kisiwani Ukerewe, Tanzania mwaka 1944. Alipokuwa akisoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwishoni mwa mwaka wa sitini alikuwa miongoni mwa waanzilishi wa *mtiririko* (mashairi-huru). Wakati huo huo aliandika riwaya yake ya kwanza ya *Rosa Mistika* (1971) iliyopigwa marufuku kwa sababu ilionekana kuwa na kashfa. Alimaliza masomo ya uzamivu Marekani (Chuo Kikuu cha Wisconsin - 1985). Wakati wa kazi yake ya uprofesa (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Gaborone, Botswana), alichapisha vitabu vingi vya ushairi, hadithi fupi, riwaya na tamthiliya moja.

**Abdilatif Abdalla** è nato a Mombasa, in Kenya, nel 1946. In seguito alla stampa del suo scritto *Kenya: Dove andiamo?* fu rinchiuso per tre anni in carcere (1969-72). Durante la prigionia scrisse la sua famosa raccolta di poesie *La voce dell'agonia* (1973). In seguito ha continuato a scrivere poesie e saggi, raccolti in varie riviste, miscellanee e antologie. Ottenuta la libertà, Abdalla andò in esilio a Dar es Salaam, insegnando all'Università. In seguito ha lavorato a Londra per la BBC, prima di trasferirsi definitivamente in Germania dove fino al pensionamento ha insegnato swahili all'Università di Lipsia.

**Euphrase Kezilahabi** è nato nel villaggio di Namagondo sull'isola di Ukerewe, nel Lago Vittoria, in Tanzania, nel 1944. Durante i suoi studi presso l'Università di Dar es Salaam, nella seconda metà degli anni Sessanta, fu tra i caposcuola del *mtiririko* (poesia in versi liberi). Proprio in quel tempo scrisse il suo primo romanzo *Rosa Mistika* (1971), che fu censurato poco dopo perché considerato scandaloso. Si è addottorato nel 1985 negli Stati Uniti presso l'Università del Wisconsin con una tesi in filosofia e critica letteraria africana. In seguito ha insegnato presso le università di Dar es Salaam e Gaborone, pubblicando numerosi testi: collezioni di poesie, romanzi, racconti e un'opera teatrale.



Università degli studi di Napoli  
"L'Orientale"

## USHAIRI NA UHURU

Poesie scelte di Abdilatif Abdalla e Euphrase Kezilahabi  
Mkusanyo wa tungo za Abdilatif Abdalla na Euphrase Kezilahabi

Curatori e Traduttori

Wahariri na Wafasiri  
Flavia Aiello e Roberto Gaudio



*Tunatabaruku kazi hii kwa mwenzetu na rafiki mpendwa,  
Jean de Dieu Karangwa*





Università degli studi di Napoli  
**"L'Orientale"**

# **USHAIRI NA UHURU**

**Poesie scelte di Abdilatif Abdalla e Euphrase Kezilahabi**  
**Mkusanyo wa tungo za Abdilatif Abdalla na Euphrase Kezilahabi**

Curatori e Traduttori

Wahariri na Wafasiri

Flavia Aiello e Roberto Gaudio

NAPOLI  
2017

# Yaliyomo

<b>Shukrani</b> .....	6
<b>Dibaji</b> .....	8
<b>Utangulizi wa Wahariri na Wafasiri</b> .....	12
<b>Utangulizi wa M.M. Mulokozi</b> .....	16
<b>Picha (1977-1978)</b> .....	41

## **Tungo za A. Abdalla na tafsiri yao kwa Kiitaliano**

<b>ya F. Aiello</b> .....	45
N'shishiyelo ni Lilo .....	46
Tuza moyo.....	54
Kuno Kunena ( <i>tafsiri ya M. Grasso kwa Kinapolitano</i> ).....	56
Siwati .....	58
Mamba .....	60
Nakukumbuka .....	62
N'sharudi .....	64
Ukurasa bikira ( <i>haijachapishwa kitabuni</i> ) .....	66

## **Tungo za E. Kezilahabi na tafsiri yao kwa Kiitaliano**

<b>ya R. Gaudioso</b> .....	69
Fasihi.....	70
Jinamizi.....	74
Fungueni Mlango.....	78
Wimbo wa mlevi ( <i>tafsiri ya M. Grasso kwa Kinapolitano</i> )...	80
Safari .....	82
Kuishi .....	84
Wakati Fulani.....	86
Wimbo wa Unyago.....	90
Dikteta.....	94
Kirudi kina shaka, shuku na kero ( <i>haijachapishwa kitabuni</i> )...	96

# Indice

<b>Ringraziamenti</b> .....	7
<b>Premessa</b> .....	9
<b>Introduzione dei curatori e traduttori</b> .....	13
<b>Introduzione di M.M. Mulokozi</b> .....	17
<b>Foto (1977-1978)</b> .....	41
<b>Poesie di A. Abdalla e traduzioni in italiano</b>	
<b>di F. Aiello</b>	45
A Questo io mi afferro .....	47
Placa l'animo .....	55
Questo parlare/'O pparlà ( <i>M. Grasso</i> ).....	57
Non mollo .....	59
Il coccodrillo .....	61
Ti ricordo.....	63
Son tornato .....	65
Pagina vergine ( <i>inedito</i> ) .....	67
<b>Poesie di E. Kezilahabi e traduzioni in italiano</b>	
<b>di R. Gaudioso</b>	69
Letteratura .....	71
Incubo .....	75
Aprite la porta.....	79
La canzone dell'ubriacone/'O mbriaco ( <i>M. Grasso</i> ).....	81
Il viaggio.....	83
Vivere .....	85
Un certo tempo .....	87
Canzone dell'Unyago .....	91
Il dittatore.....	95
Dubbio, sospetto e tormento nel ritorno ( <i>inedito</i> ) .....	97

## Shukrani

Shukrani zetu za dhati ziwaendee washairi Abdilatif Abdalla na Euphrase Kezilahabi waliotusaidia katika kazi yetu kwa kuturuhusu kuchapisha tafsiri ya Kiitaliano ya baadhi ya tungo zao. Vilevile tunawashukuru kwa picha zilizomo kwenye kitabu hiki na kwa kutupatia tungo ambazo hazijachapishwa kitabuni.

Tunatoa shukrani zetu kutoka moyoni kwa Profesa Mugyabuso Mlinzi Mulokozi (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam) aliyeandika utangulizi wa mashairi.

Mshairi Mimmo Grasso alitafsiri kwa Kinapoletano tungo mbili: *Kuno Kunena* ('O pparlà) ya Abdilatif Abdalla na *Wimbo wa mlevi* ('O mbriaco) ya Euphrase Kezilahabi. Ahsante sana.

Tunapenda kutoa shukrani zetu kwa Profesa Elena Bertoncini Zúbková ambaye hututia moyo na hutushauri mara kwa mara. Ahsante kwa kupitia tafsiri zetu za mashairi yaliyomo humu.

Tunamshukuru sana Bi. Gaudensia Emanuel (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam) alyepitia matini zetu za Kiswahili.

Hata hivyo, upungufu wowote katika uandishi ni wetu.

## Ringraziamenti

Ringraziamo di cuore i poeti Abdilatif Abdalla e Euphrase Kezilahabi per aver sostenuto il nostro lavoro permettendoci di pubblicare la traduzione italiana delle loro poesie, per averci fornito le foto che appaiono nel presente volume e per averci dato un loro testo da tradurre mai pubblicato in volume.

I nostri sinceri ringraziamenti vanno al Prof. Mugyabuso Mlinzi Mulokozi (Università di Dar es Salaam) che ha curato il saggio introduttivo alle poesie.

Ringraziamo sinceramente il poeta Mimmo Grasso per le traduzioni in napoletano delle poesie *Kuno Kunena* ('O pparlà) di Abdilatif Abdalla e *Wimbo wa mlevi* ('O mbriaco) di Euphrase Kezilahabi.

Ringraziamo con affetto la Prof.ssa Elena Bertoncini Zúbková per la sua costante vicinanza e per la sua attenta rilettura delle traduzioni delle poesie.

I nostri ringraziamenti alla dott.ssa Gaudensia Emanuel (Università di Dar es Salaam) per la revisione dei nostri testi swahili.

Ad ogni modo, qualsiasi imperfezione è da imputare solo a noi.



## Dibaji

Kitabu hiki cha tafsiri ya Mashairi ya Euphrase Kezilahabi na Abdilatif Abdalla ni muhimu sana katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili hususan Ushairi wa Kiswahili katika kipindi hiki ambapo fasihi ya Kiswahili imevuka mipaka ya jamii ya wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili na kutandawaa katika mawanda mapana ya wapenzi wa ushairi duniani. Kwa hiyo ni wazi kuwa ni kitabu ambacho kitaendeleza juhudi za kueneza fasihi ya Kiswahili duniani. Aidha, ni kitabu kinachoweza wazi historia ya Ushairi wa Kiswahili hususan katika msisitizo wa mashairi ya kimapokeo na yale ya kisasa. Kwa upande mwingine, waandishi hawa wawili wanaweka bayana matumizi ya Kiswahili cha lahaja ya Kimvita – Abdalla na Kiswahili Sanifu - Kezilahabi. Matumizi haya ya lahaja yanaonesha utajiri uliopo katika fasihi ya Kiswahili na yanachochea uchunguzi zaidi kuhusu lahaja za Kiswahili hususan katika eneo la fasihi.

Kwa hakika kitabu hiki ni juhudi za wanataaluma kutoka Chuo Kikuu cha Napoli kwa kutambua mchango wa wataalamu hawa wa Kiswahili hususan katika Ushairi wa Kiswahili. Mchango wao umejidhihirisha wazi katika mashairi yatakayosomwa katika kitabu hiki. Ushirikiano kati ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (CKD) na Chuo Kikuu cha Napoli (UNIOR) ulianza zaidi ya miaka kumi na tano iliyopita. Ni ushirikiano ambao kwa hakika umekuwa na mafanikio makubwa. Ingawa Taasisi ya Taaluma za Kiswahili ya CKD ambayo ndiyo inahusika moja kwa moja na ushirikiano huu ina mikataba mingi ya ushirikiano, kazi zilizofanyika kupitia mkataba huu ni za kujivunia na zinaonekana bayana. Kwa kuwa si rahisi kuyataja mambo yote yaliyofanyika, mambo machache yatabainishwa ili kutoa picha kwa wasomaji.

Mbali na mafanikio haya ya kitabu, mara baada ya Mkataba wa Ushirikiano kati ya vyuo hivi viwili kuanzishwa mwaka 2002; miongoni mwa mambo yaliyopewa kipaumbele ni kubadilishana wanataaluma ili kupanua wigo wa kujifunza mambo mbalimbali yanayofanyika katika vyuo hivi viwili; kuandaa miradi ya utafiti kuhusu lugha ya Kiswahili na Fasihi pamoja na kubadilishana wanafunzi kwenda kusoma kwa muda mfupi na/au kufanya utafiti. Kwa hakika mipango hii imefanikiwa kwa kiasi kikubwa. Mathalani, kutokana na utaratibu wa

## Premessa

Questo libro di traduzioni delle poesie di Euphrase Kezilahabi e Abdilatif Abdalla è di gran valore per la diffusione della letteratura swahili, e in particolare della poesia, in un'epoca come quella attuale in cui questa ha valicato i confini della comunità dei locutori della lingua e ha cominciato a farsi conoscere dagli appassionati di poesia nel mondo. È chiaro, quindi, che questo libro contribuisce a diffondere la letteratura swahili nel mondo e, al tempo stesso, fa emergere, attraverso la scelta di poesie tradizionali e moderne, la storia della poesia swahili. Inoltre, queste poesie mostrano diversi usi della lingua swahili, il dialetto Kimvita (Abdalla) e lo standard swahili (Kezilahabi). L'utilizzo di queste varietà mette in risalto l'eterogeneità della letteratura swahili, che esige ulteriori ricerche.

Questo libro dimostra l'impegno dei ricercatori dell'Università degli Studi di Napoli "L'Orientale" nel far conoscere il contributo di questi due scrittori swahili. La cooperazione tra l'Università di Dar es Salaam (UDSM) e l'Università degli Studi di Napoli "L'Orientale" (UNIOR) è iniziata oltre quindici anni fa. E' una cooperazione che ha avuto senz'altro buoni risultati. Anche se il Dipartimento di Studi Swahili, che è il diretto referente della convenzione presso l'Università di Dar es Salaam, ha molti accordi di cooperazione, il lavoro che viene svolto nell'ambito di questo accordo è evidente e degno di lode. Non è semplice menzionare tutto ciò che è stato svolto in questi anni, ci limiteremo qui a sintetizzare brevemente la storia della nostra convenzione.

Questo libro non è il primo frutto della nostra cooperazione. A partire dalla stipula dell'accordo tra le due università, nel 2002, è stata data priorità allo scambio docenti/ricercatori, al fine di aggiornarsi sulle diverse ricerche e attività in corso nelle due università, e allo sviluppo di progetti di ricerca sulla lingua e letteratura swahili. Inoltre, importante elemento di questo accordo è lo scambio studenti, per motivi di studio e/o di ricerca. Senz'altro questi obiettivi sono in gran parte riusciti. Ad esempio, hanno partecipato al programma di mobilità circa 12 studenti e 14 docenti provenienti dai due istituti, per seguire le attività previste nell'accordo. Gli studenti in mobilità hanno potuto studiare per la durata di circa un semestre e/o svolgere ricerche

kubadilishana wanafunzi, takribani wanafunzi 12 na walimu 14 kutoka katika vyuo hivi wameweza ama kuja CKD au kwenda UNIOR kwa shughuli zilizobainishwa katika mkataba wa ushirikiano. Wanafunzi waliohusika katika mtagusano huu waliweza ama kusoma kwa semesta moja na/au kufanya utafiti katika kiwango cha Uzamili. Miongoni mwa wanafunzi kutoka UNIOR waliokuja CKD kufanya utafiti ni Ciro Marzio (2004), Maria Suriano (2006) na Roberto Gaudio (2015). Baadhi ya wanafunzi waliosoma kwa semesta moja CKD kutoka UNIOR ni Sara Centrella (2008), Rosanna Tramutoli (2009), Roberto Gaudio (2010), Cristina Nicolini (2014), Valeria Del Vasto (2015) na Emiliano Minerba (2016). Kwa upande wa wanataaluma walioshiriki katika shughuli mbalimbali za ushirikiano kama vile miradi ya kitaaluma, warsha na semina ni pamoja na Prof. Mlinzi Mulokozi, Prof. John Kiango, Prof. Fikirini Senkoro, Prof. Aldin Mutembei, Dkt. Selemani Sewangi, Dkt. Ernesta Mosha, Dkt. Shani Omari na Mwl. Angelus Mnenuka kutoka CKD. Kutoka UNIOR ni pamoja na Mwl. Abeid Tandika, Prof Sergio Baldi, Dkt. Patrizia Zotti na Dkt. Flavia Aiello.

Pia, miradi mbalimbali ya pamoja imeweza kuanzishwa. Baadhi ya miradi inayoanzishwa ni uandaaji wa kongoo matini ya Kiswahili – Kiitaliano na uandishi wa kitabu kuhusu fasihi simulizi ya Kimtang’ata. Kitabu hiki cha fasihi simulizi ambacho kinaandikwa kwa lugha ya Kiswahili kitakuwa ni hazina ya marejeleo kuhusiana na lahaja ya Kimtang’ata na fasihi simulizi kwa ujumla; na hivyo kuongeza wingi wa vitabu vinavyohitajika sana kuhusu simulizi za Kiafrika na utafiti kuhusu lahaja. Kwa hakika ushirikiano huu utaendelea kuwa chachu kwa wanataaluma wa vyuo hivi viwili na wanajamii kwa nchi hizi mbili katika kuchochea maendeleo ya kitaaluma hususan ya lugha na fasihi ya Kiswahili. Ama kweli umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.

Ernesta S. Mosha (PhD)

*Mkurugenzi, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili  
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

per la tesi di laurea specialistica. Tra gli studenti UNIOR venuti presso l'UDSM a fare ricerca vi sono *Ciro Marzio (2004)*, *Maria Suriano (2006)* e *Roberto Gaudio (2015)*. Tra gli studenti UNIOR che hanno frequentato i corsi dell'UDSM per un semestre citiamo *Sara Centrella (2008)*, *Rosanna Tramutoli (2009)*, *Roberto Gaudio (2010)*, *Cristina Nicolini (2014)*, *Valeria Del Vasto (2015)* e *Emiliano Minerba (2016)*. Tra i docenti che hanno collaborato nel quadro di diverse attività, quali progetti di ricerca, workshop e seminari, figurano, dall'UDSM, il prof. *Mlinzi Mulokozi*, il prof. *John Kiango*, il prof. *Fikirini Senkoro*, il prof. *Aldin Mutembei*, il dott. *Selemani Sewangi*, la dott.ssa *Ernesta Masha*, la dott.ssa *Shani Omari* e il docente *Angelus Mnenuka*, dall'UNIOR il lettore *Abeid Tandika*, il prof. *Sergio Baldi*, la dott.ssa *Patrizia Zotti* e la dott.ssa *Flavia Aiello*.

Inoltre, diversi progetti comuni sono stati avviati. Tra i progetti in corso, vi è la preparazione di un corpus testuale Swahili – Italiano e la stesura di un volume sulla letteratura orale nel dialetto Kimtang'ata. Quest'ultimo, redatto in swahili, costituirà un prezioso riferimento bibliografico per quanto riguarda il Kimtang'ata e la letteratura orale swahili, che riteniamo importante per la ricerca sulla letteratura orale africana e sui dialetti. Senza dubbio la nostra cooperazione continuerà a coinvolgere studiosi delle due università, la società civile dei due paesi, e a promuovere ricerche comuni, in particolare sulla lingua e letteratura swahili. E' proprio vero che l'unione fa la forza, la divisione rende deboli.

*Ernesta S. Masha (PhD)*  
*Direttrice, Dipartimento di Studi Swahili*  
*Università di Dar es Salaam*

## Utangulizi wa wahariri na wafasiri

Chimbuko la kitabu hiki ni mazungumzo yetu kuhusu ushairi wa Kiswahili na upana wake, pamoja na wazo la kuwafikishia wasomaji wa Kiitaliano mifano ya utajiri wa sanaa ya Kiswahili. Kwa hiyo tumechagua kutafsiri kwa Kiitaliano tungo za washairi wawili wenye asili na mtindo tofauti: Abdilatif Abdalla na Euphrase Kezilahabi. Abdalla anatoka Mombasa, pwani ya Kenya, na hutunga kufuatana na arudhi ya kimapokeo ya Kiswahili. Kezilahabi anatoka Ukerewe, Tanzania bara, na hutunga *mtiririko* akiwa ameathirika na fasihi simulizi ya Kikerewe na fasihi ya kigeni. Kazi za kishairi za Kezilahabi zilianzisha mgogoro kati ya “wanamapokeo” na “wanausasa” ulioendelea kwa muda mrefu na lengo letu kwa sasa sio kuuendeleza mjadala huo wala kuurahisisha, tuna imani kuwa tofauti hizi ni sehemu ya utajiri wa ushairi wa Kiswahili. Aidha, mjadala juu ya mtindo wa ushairi ulikuwa umehusishwa na ule wa utambulisho wa Kiswahili, ila sio lengo letu kujadili suala zito kama hilo kwenye utangulizi huu mfupi. Tunachokisisitiza hapa ni ubora na uzuri wa ushairi wa Kiswahili kwa ujumla pamoja na umuhimu wa kuusambaza duniani kupitia lugha mbalimbali.

Ndani ya mkusanyo huu kuna tafsiri mbili za mshairi Mimmo Grasso kwa Kinapolitano. Mimmo Grasso alitafsiri tungo ya “Kuno Kunena” ya A. Abdalla na ya “Wimbo wa Mlevi” ya E. Kezilahabi kutokana na tafsiri zetu za Kiitaliano. Kwa ujumla, mtindo wake wa kutafsiri ulikuwa wa kutunga upya, yaani tafsiri zake zilihamisha matini chanzi kwenye lugha na utamaduni vya Kinapolitano. Hata hivyo, mara kwa mara tafsiri ya Kinapolitano yanaonyesha kuwa karibu zaidi na maneno ya Kiswahili, kwa mfano mfasiri alitafsiri usemi wa Kiswahili “maji ya kunde” kwa kutumia picha ya rangi ya maji inayotokana na weupe wa maharage yanayozama ndani yake. Tunaona kwamba kuwepo kwa tafsiri ya Kinapolitano ndani ya mkusanyo huu zinasaidia kuhusisha kitabu hiki na mazingira ya kijamii yanayozunguka Chuo Kikuu cha Napoli “L’Orientale”.

Maamuzi yetu juu ya tafsiri ya tungo zilizokusanywa humu ni kuwasilisha tofauti baina ya mitazamo na mitindo yao ya kishairi. Ndiyo maana tumejaribu kutafsiri tukitazama sifa za kipekee za kishairi za matini tulizozichagua. Kwa hiyo tungo za Abdilatif Abdalla

## Introduzione dei curatori e traduttori

Questo libro è nato dai nostri discorsi intorno alla poesia swahili, alla sua complessità, e dal desiderio di comunicare al pubblico italiano parte della ricchezza della poesia swahili. Abbiamo scelto, quindi, di tradurre in italiano i componimenti di due poeti d'origine e stile diversi: Abdilatif Abdalla e Euphrase Kezilahabi. Abdalla viene da Mombasa, metropoli costiera del Kenya, e scrive seguendo la prosodia classica swahili. Kezilahabi proviene dall'isola di Ukerewe, nella zona continentale della Tanzania, e scrive *mtiririko* (poesia in versi liberi) influenzato dalla letteratura orale di Ukerewe e dalla letteratura straniera. Le poesie di Kezilahabi sono state la miccia che ha innescato un lungo dibattito, ancora vivo, tra “tradizionalisti” e “riformisti”; non è nostra intenzione continuarlo né semplificarlo: crediamo che queste diversità siano parte della ricchezza della poesia swahili. Per la verità questo dibattito più che sugli stili della poesia swahili verte sull'identità swahili e non è nostra intenzione soffermarci su tale punto in questa breve introduzione. Ciò che ci preme qui affermare è la qualità e la bellezza della poesia swahili e l'importanza di tradurla in diverse lingue.

La presente raccolta contiene due lavori del poeta Mimmo Grasso che si pongono a metà strada tra una traduzione e una riscrittura in napoletano di due poesie, una per ogni autore scelto. Mimmo Grasso ha lavorato partendo dalle nostre traduzioni in italiano. Il suo lavoro, seppure abbia le caratteristiche della riscrittura, quali per esempio un trasferimento degli elementi originali nella lingua e cultura napoletana, d'altra parte tende alla lettera. Ad esempio, l'espressione swahili “*maji ya kunde*” (acqua di fagioli) che si riferisce al colore di una pelle non molto scura, è stata tradotta “*l'acqua chiara/ addò se spogna 'o gghianco r' 'e fasule*” (l'acqua chiara/ dov'è in ammollo il bianco dei fagioli). La scelta del napoletano significa per noi un tentativo di stabilire connessioni con il territorio circostante, dove ha sede l'Università degli Studi di Napoli “L'Orientale”.

La nostra scelta, quindi, è mostrare due poetiche differenti ma non antitetiche. Per questo la nostra traduzione tenta di restituire in italiano le peculiarità delle poesie originali. I componimenti di Abdilatif Abdalla sono stati tradotti rispettando la metrica e le rime degli

zimetafsiriwa kulingana na mpangilio ule ule wa vina na mizani, ila ilikuwa ni vigumu kuhifadhi lugha ya kilahaja ya Kimvita. Hata hivyo mfasiri amejaribu kutumia lugha inayosawiri dhahiri na ghadabu katika ujumbe wake. Vilevile tafsiri za tungo za Euphrase Kezilahabi zina ari ya kufikisha nguvu ya sitiari, sauti na mahadhi ya matini zake kwa kuhamisha kwa Kiitaliano mpangilio wa maneno. Mfasiri amejaribu kufuata lugha ya mwandishi ambaye anatumia maneno yanayofanana na mazungumzo ya kawaida kwa kuzingatia falsafa yake. Mikakati ya kitafsiri ya wafasiri inafanana, yaani wote wawili hawakutaka kuhamishia matini chanzi kwenye lugha na utamaduni wa Kiitaliano bali walijaribu kutajirisha matini yao ya Kiitaliano na nguvu ya kishairi ya matini chanzi.

Tunatumaini kuwa tumeweza kufikia angalau nusu ya lengo letu la kuunganisha fasihi za lugha na tamaduni tofauti kwa njia ya ‘nguvu ya kishairi’. Kama ni hivyo, inathibitisha kuwa kuna uwezekano wa kulinganisha na kuunganisha kazi mbalimbali za sanaa, basi hatuoni sababu ya kutowalinganisha Abdilatif Abdalla na Euphrase Kezilahabi. Mbali na tofauti nyingi baina ya watunzi hawa, sisi tunaona kwamba hata mahusiano si haba, yaani wote wawili wameshuhudia ushairi, ukweli na uhuru kama wajibu wa mshairi na, vilevile, katika tungo zao maisha na matendo ya kila siku yanachukua nafasi kubwa, hasa hisia za maumivu.

Picha zilizochapishwa humu zinaonyesha pia uhusiano wa kipekee kati yao. Picha hizi zinasimulia kuhusu wakati ule na mahali pale: Dar es Salaam ya miaka ya sabini. Wakati huo unahitaji kuchunguzwa zaidi hasa upande wa historia, utamaduni na ujumi. Licha ya hayo, picha hizo zinashuhudia mahusiano kati ya pande mbili, mazungumzo yanayotakiwa kuongezwa na kuendelezwa hasa kwa wakati huu.

originali, ma non il particolare uso del dialetto swahili di Mombasa (Kimvita). Ciò nonostante, la traduttrice ha provato a trasmettere l'immediatezza e la visceralità dei versi di Abdalla. La traduzione delle poesie di Euphrase Kezilahabi, prestando attenzione parola per parola, aspira a trasmettere in italiano la forza delle metafore, del suono e del ritmo dell'originale. Il traduttore ha tentato di seguire l'autore in tutte le sue scelte linguistiche, anche le più singolari, perché nella poetica di Kezilahabi stile e filosofia sono un connubio inscindibile. Le strategie traduttologiche dei due curatori, quindi, si assomigliano; per entrambi lo scopo non era trasferire il testo originale nella lingua e cultura italiana ma tentare di arricchire i testi in italiano della potenza poetica degli originali.

Speriamo di aver adempiuto almeno in parte al compito che ci siamo proposti: unire poeticamente due lingue e tradizioni diverse. Se l'abbiamo fatto è grazie alla possibilità che ogni arte ha di unire e d'essere sempre aperta al confronto, quindi ci pare ancor meno peregrino confrontare e unire le esperienze poetiche di Abdilatif Abdalla e Euphrase Kezilahabi in questo libro. Se numerose sono le differenze tra questi autori, non da meno sono le connessioni: entrambi testimoniano l'imperativo esistenziale della poesia vissuta come ricerca di verità e libertà. Nelle loro poesie, infatti, il vissuto, l'esperienza è al centro della loro ispirazione, soprattutto l'esperienza del dolore.

Le foto che presentiamo in questo volume mostrano un rapporto personale tra i due poeti. Ci raccontano della Dar es Salaam degli anni Settanta, prolifico laboratorio politico, filosofico e artistico, su cui riteniamo resti ancora tanto da indagare dal punto di vista storico, culturale ed estetico. Queste foto, inoltre, testimoniano rapporti e dialoghi fra due parti, che specialmente in questo tempo andrebbero potenziati e promossi.



## Utangulizi wa M.M. Mulokozi

Miaka kadha iliyopita niliombwa na shirika moja la uchapishaji la Uingereza niandike maelezo kuhusu waandishi kadha muhimu wa Tanzania kwa ajili ya “Ensaklopidia ya Fasihi ya Jumuiya ya Madola” (*Commonwealth*) ambayo walikuwa wakiandaa. Niliwaeleza kuwa waandishi hao waliowataja walikuwa wakiandika kazi zao nyingi kwa lugha ya Kiswahili. Wakanijibu kuwa kama hawaandiki kwa lugha ya Kiingereza basi hawakustahili kuwamo katika chapisho lao. Nikawauliza kama walikuwa wanakusudia kuchapisha “Ensaklopidia ya Fasihi ya Jumuiya ya Madola” au “Ensaklopidia ya Fasihi ya Jumuiya ya Madola katika lugha ya Kiingereza?” Nikawafanulia kuwa Jumuiya ya Madola ilikuwa na fasihi nyingi katika lugha nyingi na si Kiingereza tu. Wakanijibu kuwa hilo hawakuwa wamelifikiria, na wakakubali kubadilisha jina la chapisho lao ili kuonesha kuwa lilihusu waandishi waandikao kwa lugha ya Kiingereza tu, si waandishi wote wa Jumuiya ya Madola. Sijui kama kitabu hicho kilichapishwa, maana sikukifuatilia zaidi.

Hata hivyo, tukio hilo lilidhihirisha tatizo la msingi kuhusu namna wataalamu wengi wa nje, na hata wa ndani waliosoma elimu ya Kimagharibi, walivyokuwa wanaitazama fasihi ya Afrika; kwao waandishi wa Kiafrika walikuwa ni kina Chinua Achebe, Flora Nwapa, Camara Laye, Wole Soyinka, Okot p’Bitek, Ngugi wa Thiong’o na wengine walioandika katika lugha za wakoloni. Waandishi kama Muyaka bin Haji, Shaaban Robert, M.S. Abdulla, E. Hussein, A. Kitereza, E. Kezilahabi na A. Abdalla hawakutambuliwa (isipokuwa na wataalamu wachache ‘viroja’ walioitwa ma-*Africanist*). Miaka ya hivi karibuni hali imeanza kubadilika. Baadhi ya wasomi wa Kiafrika wameanza kutazama ndani, kuchunguza kilichomo ndani ya lugha zetu wenyewe na kukataa kuwakilishwa na kundi dogo la wasomi ambao Ngugi wa Thiong’o aliwaita “Afro-Saxons.” Wataalamu kadha wa Ulaya na Marekani pia wameanza kuzichunguza fasihi za lugha za asili za Kiafrika kwa mtazamo mpya. Mabadiliko haya yalisukumwa sana na juhudi za Ngugi wa Thiong’o na wasomi wengine wachache za kutetea na kutumia lugha za Kiafrika. Mageuzi haya, ambayo tunaweza kuyaita mzinduko mpya wa Uafrika, yameibua mambo ambayo hayakutarajiwa

## Introduzione di M.M. Mulokozi

Alcuni anni fa una casa editrice britannica mi chiese di scrivere, per l'Enciclopedia della Letteratura del Commonwealth che stava per pubblicare, delle voci su alcuni importanti scrittori della Tanzania. Spiegai loro che gli scrittori di cui mi avevano fatto il nome avevano scritto molte opere in lingua swahili. Mi risposero che se questi scrittori non scrivevano in inglese, allora non meritavano di far parte della loro pubblicazione. Chiesi loro: intendevano pubblicare una Enciclopedia della *Letteratura* del Commonwealth oppure una Enciclopedia della Letteratura del Commonwealth scritta in inglese? Precisai che nel Commonwealth esistevano molte letterature, scritte in numerose lingue e non solo in inglese. Mi risposero che a questo non avevano pensato, ed accettarono di modificare il titolo della loro pubblicazione per mostrare che riguardava soltanto gli scrittori anglofoni, e non tutti gli scrittori del Commonwealth. Non so se il volume è poi stato pubblicato, poiché non me ne sono più curato.

Ad ogni modo, questo episodio rivela un problema di fondo riguardo alla maniera in cui molti studiosi esteri, ma anche quelli locali istruiti all'occidentale, guardavano alla letteratura dell'Africa; per loro gli scrittori africani erano Chinua Achebe, Flora Nwapa, Camara Laye, Wole Soyinka, Okot p'Bitek, Ngugi wa Thiong'o e altri che scrivevano nelle lingue dei colonizzatori. Scrittori come Muyaka bin Haji, Shaaban Robert, M.S. Abdulla, E. Hussein, A. Kitereza, E. Kezilahabi e A. Abdalla non venivano minimamente considerati (tranne che da alcuni studiosi "buffi" chiamati Africanisti). Negli ultimi anni, lo stato delle cose ha iniziato a cambiare. Alcuni intellettuali africani hanno cominciato a osservare meglio, ad approfondire quel che c'è nelle nostre proprie lingue, e a rifiutarsi di essere rappresentati da un piccolo gruppo di studiosi, che Ngugi wa Thiong'o chiama "Afro-Sassoni". Anche alcuni esperti europei e americani hanno cominciato a fare ricerca sulle letterature in lingue autoctone africane da un nuovo punto di vista. Questi cambiamenti incoraggiano molto l'impegno di Ngugi wa Thiong'o ed altri pochi intellettuali nel difendere e utilizzare le lingue africane. Questi mutamenti, che possiamo definire un nuovo risveglio dell'Africanità, hanno fatto emergere qualcosa del tutto

kabisa: ghafla ulimwengu umegundua kwamba lugha za Kiafrika zina waandishi bora na wenye ubunifu wa kipekee kabisa, pengine kuliko hata wale waliojipatia sifa na umashuhuri kutokana na kuandika katika lugha za Ulaya. Miongoni mwa waandishi hao “waliogunduliwa” ni Euphrase Kezilahabi (alizaliwa Ukerewe, Tanzania, 1944) na Abdilatif Abdalla (alizaliwa Mombasa, Kenya, 1946)

Nimefahamiana na Mwalimu Kezilahabi kwa miaka kama hamsini sasa. Tulikutana kwa mara ya kwanza mwaka 1970 katika Shule ya Sekondari ya Juu ya Mkwawa, Iringa. Nilikuwa nasoma kidato cha tano, na Kezilahabi alikuwa mmoja wa walimu wangu wa Kiswahili. Baadaye alikwenda kufundisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambako nilimkuta mwaka 1972. Aliendelea kuwa mwalimu wangu wa fasihi hadi nilipohitimu digrii ya kwanza mwaka 1975. Kezilahabi aliniathiri kisanaa katika kipindi hicho muhimu cha makuzi yangu hapo chuoni. Ingawa mimi na yeye tulitofautiana kidogo katika baadhi ya mitazamo yetu ya kisiasa na kifalsafa, lakini sanaa yake, ucheshi wake wa kimyakimya na mawazo yake kuhusu fasihi, hasa ushairi, yalinivutia. Nilikuwa kila nikitunga mashairi humpelekea akayasoma na kunipa ushauri. Mgogoro wa ushairi kati ya “wanamapokeo” na “wanausasa” ulipolipuka mwaka 1973, mimi nilijiunga upande wa Kezilahabi kutetea ‘ushairi huru’ uliokuwa ukipigwa vita na wanajadi.

Miongoni mwa washairi waliokuwa upande wa wanamapokeo ni Abdilatif Abdalla. Nilikutana naye kwa mara ya kwanza nilipojiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1972. Alikuwa akifanya kazi katika Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (ambayo sasa ni Taasisi ya Taaluma za Kiswahili), na alikuwa ni mmoja wa walimu wetu wa fasihi katika Idara ya Kiswahili. Alikuwa ndio kwanza ametoka kifungoni Kenya kutokana na harakati zake za siasa za kutetea wanyonge. Kilichonivutia kumhusu, mbali na haiba yake ya bashasha, ni mtazamo na mwelekeo wake wa kimaendeleo – unaweza kuuita wa mrengo wa kushoto – wa kisiasa na kisanaa. Nadiriki kusema kuwa Abdilatif Abdalla alikuwa na athari kubwa kwangu katika kipindi hicho cha ‘kujitafuta’ cha ujana wangu. Wakati wa mgogoro wa ushairi, mimi na Abdilatif Abdalla tulipingana bila kupigana, na urafiki wetu ulibaki palepale.

Yumkini uhusiano wangu huu na washairi hawa maarufu ndio ulionipa sifa machoni pa waandaaji wa kitabu hiki ya kustahili

inatteso: all'improvviso il mondo ha scoperto che le lingue africane presentavano eccellenti scrittori, con una creatività assolutamente unica, a volte forse più di autori divenuti famosi e apprezzati per il fatto di scrivere in lingue europee. Tra gli scrittori che sono stati "scoperti" vi sono Euphrase Kezilahabi (nato a Ukerewe, Tanzania, 1944) e Abdilatif Abdalla (nato a Mombasa, Kenya, 1946).

Conosco *Mwalimu*<sup>1</sup> Kezilahabi da circa cinquant'anni. Ci siamo incontrati per la prima volta nel 1970 nella scuola superiore Mkwawa, a Iringa. Io ero al quinto anno, e Kezilahabi era uno dei miei professori di Swahili. In seguito è divenuto docente presso l'Università di Dar es Salaam, dove l'ho trovato nel 1972. È stato il mio professore di Letteratura fino a quando non ho terminato il primo corso di studi (B.A.) nel 1975. Kezilahabi ha avuto una grande influenza su di me dal punto di vista artistico, nell'importante periodo della mia formazione presso questa università. Anche se tra di noi esistevano delle differenze riguardo alle nostre opinioni politiche e filosofiche, mi affascinarono molto la sua arte, il suo laconico senso dell'umorismo e le sue idee sulla letteratura, in particolare sulla poesia. Ogniqualvolta componevo delle poesie gliele facevo leggere e lui mi dava dei consigli. Nel 1973, quando si scatenò la disputa tra poeti "tradizionalisti" e "modernisti", io mi schierai dalla parte di Kezilahabi nel difendere la "poesia libera" [*ndt* in versi liberi] che veniva criticata dai tradizionalisti.

Tra i poeti dalla parte dei tradizionalisti vi era Abdilatif Abdalla. L'ho incontrato per la prima volta quando mi sono iscritto all'Università di Dar es Salaam nel 1972. Lavorava presso l'Istituto di Ricerca Swahili (che oggi è stato rinominato Istituto di Studi Swahili), ed era uno dei nostri professori di Letteratura nel Dipartimento di Swahili. Era appena uscito dal carcere in Kenya, dove era stato rinchiuso a causa del suo attivismo politico nel difendere i diritti degli oppressi. Quel che mi affascinava di lui, oltre alla sua personalità allegra e cordiale, era il suo modo di pensare e il suo orientamento progressista – chiamiamolo di sinistra – in politica e nell'arte. Posso affermare che Abdilatif Abdalla ha avuto una grande influenza su di me nel periodo in cui "ceravo me stesso", durante la mia gioventù. All'epoca della disputa sulla poesia swahili, io e Abdilatif Abdalla ci scontrammo, ma senza ostilità, senza mai intaccare la nostra amicizia.

kuteuliwa kuwa mwandishi wa Utangulizi huu. Lakini hiyo ni siri yao. Sasa tuangalie mkusanyo wenyewe.

Kabla ya kuuzungumzia mkusanyo huu, yafaa nieleze hapa kuwa Euphrase Kezilahabi na Abdilatif Abdalla ni washairi waliochambuliwa na kuhakikiwa sana miaka ya karibuni na magwiji wa fasihi wa ndani na nje ya Afrika Mashariki. Vitabu, makala na tasnifu nyingi zimeandikwa kuhusu kazi zao. Sitamani na sikusudii kujiunga na magwiji hao katika Utangulizi huu mfupi. Hivyo maelezo nitakayoyatoa hapa ni ya kinafsi, yenye kubeba hisia na maono yangu kuhusu tungo za washairi hawa, uhusiano wao na muktadha wa kijamii-kihistoria wa nchi zetu, na mchango wao katika maendeleo ya kisanaa na kifikra ya fasihi ya Kiswahili.

Mashairi yaliyomo katika mkusanyo huu yamechukuliwa katika mikusanyo mitatu ya Euphrase Kezilahabi na diwani moja ya Abdilatif Abdalla. Mikusanyo ya Kezilahabi ni *Kichomi* (kilichochapishwa na Heinemann, Nairobi, mwaka 1973), *Karibu Ndani* (kilichochapishwa na Dar es Salaam University Press, Dar es Salaam, mwaka 1988) na *Dhifa* (kilichochapishwa na Vide-Muwa, Nairobi, mwaka 2008). *Kichomi* ndio mkusanyo wa kwanza kabisa wa tungo za Kezilahabi. Ni chapisho lililomtambulisha Kezilahabi kuwa mtunzi wa mkondo mpya wa ushairi katika fasihi ya Kiswahili, siyo kifani tu (hakuzingatia urari wa vina na mizani) bali hata kifikra. Tutaeleza zaidi baadaye kuhusu mambo haya. Mbali na vitabu hivyo, Kezilahabi amechapisha pia riwaya nne za kihalisia, mbili (*Nagona* na *Mzingile*) za ukiushihalisia (au uhalisiamazingaombwe), tamthilia moja, hadithi fupi kadha na insha nyingi za kitaaluma kuhusu fasihi. Tasnifu yake ya Udaktari wa Falsafa kuhusu “Falsafa ya Kiafrika na Suala la Uchaganuzi wa Kifasihi” (Chuo Kikuu cha Wisconsin-Madison, 1985) inatufunulia undani wa maono yake kuhusu uhusiano wa falsafa (ya Kiafrika na ya ulimwengu) na fasihi, na ina mchango muhimu katika nadharia ya fasihi. Kimsingi, anapendekeza uhakiki wa Kiafrika ujikite katika ontolojia ya Mwafrika, utazame ndani na nje ya Afrika, ujielekeze mbele badala ya kurejea nyuma, na ulenge katika kumkomboa Mwafrika. Na kama ambavyo tungo zake za kishairi zilituanzishia mkondo mpya wa ushairi wa Kiswahili, riwaya zake za *Nagona* na *Mzingile* zimetuanzishia mkondo mpya wa bunilizi. Na mikondo yote miwili tayari imepata wafuasi na waigaji wengi. Katika Utangulizi

Probabilmente il mio rapporto con questi due famosi poeti è proprio ciò che ha spinto i curatori di questo libro a chiedermi di scrivere un saggio introduttivo. Chissà. Ma veniamo alla raccolta di poesie.

Prima di venire al dunque, è bene spiegare che negli ultimi tempi i poeti Euphrase Kezilahabi e Abdilatif Abdalla sono stati spesso studiati e analizzati da esperti in Africa orientale e all'estero. Molti libri, articoli e tesi sono stati scritti sulle loro opere. Non è mio desiderio né mia intenzione fare lo stesso tipo di lavoro in questa breve introduzione. Le spiegazioni che qui esporrò sono del tutto personali, esprimono le mie sensazioni e i miei pensieri sui componimenti di questi due poeti, il loro rapporto con il contesto sociale e storico dei nostri paesi, e il loro contributo allo sviluppo artistico e intellettuale della letteratura swahili.

Le poesie che appaiono in questo libro sono state scelte da tre raccolte di Euphrase Kezilahabi e una di Abdilatif Abdalla. Le raccolte di Kezilahabi sono *Kichomi (Dolore dilaniante)*, ed. Heinemann, Nairobi, 1973), *Karibu Ndani (Benvenuto a casa)*, ed. Dar es Salaam University Press, 1988) e *Dhifa (Banchetto)*, ed. Vide-Muwa, Nairobi, 2008). *Kichomi* è in assoluto la prima raccolta poetica di Kezilahabi. È la pubblicazione che fece conoscere Kezilahabi quale promotore di una nuova corrente poetica nella letteratura swahili, non solo dal punto di vista stilistico (non si atteneva alla regolarità della rima e della metrica), ma anche dal punto di vista concettuale. Spiegherò meglio più avanti questi aspetti. Oltre a queste raccolte poetiche, Kezilahabi ha pubblicato quattro romanzi realisti, due (*Nagona* e *Mzingile*) nello stile del realismo magico, un'opera teatrale, alcuni racconti brevi e molti saggi letterari. La sua tesi di dottorato su "La filosofia africana e la questione dell'interpretazione letteraria" (Università di Wisconsin-Madison, U.S.A., 1985) ci rivela la profondità del suo pensiero sul rapporto tra filosofia (africana e mondiale) e letteratura, e costituisce un importante contributo alla teoria della letteratura. Fondamentalmente, egli suggerisce che la critica letteraria africana si focalizzi sull'ontologia dell'Africano, che guardi dentro e fuori l'Africa, che si diriga in avanti piuttosto che tornare indietro, e che miri a liberare l'Africano. E così come i suoi componimenti poetici hanno dato inizio a una nuova corrente di poesia swahili, i suoi romanzi *Nagona* e *Mzingile* hanno inaugurato una nuova corrente di prosa creativa. Ed entrambe queste correnti hanno già richiamato molti seguaci ed imitatori. In questa breve introduzione non saranno discusse tutte le opere di Kezilahabi, ci concentreremo soltanto sulla sua poesia.

huu mfupi hatutazungumzia kazi zote za Kezilahabi bali tutajikita katika ushairi wake tu.

Ama kuhusu Abdilatif Abdalla, mbali na diwani yake adhimu ya *Sauti ya Dhiki* (iliyochapishwa na Oxford University Press, Nairobi, mwaka 1973) ambayo imetupatia mashairi yaliyomo katika mkusanyo huu, yeye pia ni mwandishi na mwanazuoni mahiri ambaye ameandika tenzi, mashairi (yaliyochapishwa katika magazeti na majarida) na insha nyingi. Insha zake kadha zinahusu dhima ya ushairi katika jamii, na mtazamo wake kuhusu sanaa ya ushairi. Kama ambavyo Kezilahabi amethibitisha kuwa ushairi huru unaweza kupendeza na kubeba fikra nzito, Abdilatif Abdalla amethibitisha kuwa ushairi wa kimapokeo bado una mvuto wa kisanaa na uwezo wa kubeba mawazo mapya ya kisasa. Kilicho muhimu ni kipaji na umakini wa mshairi mwenyewe.

Tungo za Kezilahabi na Abdilatif Abdalla ziliibuka katika kipindi cha vuguvugu la ujenzi wa jamii mpya 'huru' baada ya ukoloni wa Kimagharibi wa miongo kadha nchini Tanzania na Kenya. Migogoro na mivutano ya kijamii na kisiasa (kikabila, kitabaka, kiuchumi, kivyama, kidini) ya miaka ya sitini na baadaye ndiyo iliyoibua mashairi ya E. Kezilahabi na A. Abdalla yaliyomo katika diwani hii.

Mikusanyo mitatu ya Kezilahabi inabainisha vipindi vitatu vya historia ya Tanzania baada ya Uhuru. Kipindi cha kwanza, cha kuanzia mwaka 1961 hadi kama 1970, kilikuwa ni cha kusherehekea na kushangilia Uhuru, na papo hapo kutafakari maana ya Uhuru huo na aina ya jamii inayotakiwa kujengwa. Mgawanyiko wa kijamii na kitabaka ulikuwa umeanza kujitokeza, viongozi walioshika hatamu walianza kujitajirisha huku wananchi walio wengi wakizidi kufukarika na kulalamika. Liliibuka kundi la watu walioitwa *Wabenzi* (wenye kumiliki au kutumia magari ya anasa ya aina ya *Mercedes Benz*) ambao walijinufaisha kwa rasilimali za nchi na serikali bila kujali hali ya wanyonge. Kufikia mwaka 1967, Chama tawala kilichoongozwa na Mwalimu J.K. Nyerere kilishtuka na kuona kwamba nchi ilikuwa inakwenda pabaya; kulihitajika mtazamo na mwelekeo mpya ili kudumisha umoja na uzalendo. Mwezi Februari mwaka huo likazaliwa Azimio la Arusha lililoiweka Tanzania kwenye njia ya kuelekea kwenye Ujamaa na Kujitegemea.

Riguardo Abdilatif Abdalla, oltre alla sua splendida raccolta poetica *Sauti ya Dhiki* (*La voce dell'agonia*, ed. Oxford University Press, Nairobi, 1973) da cui provengono le poesie scelte per questa pubblicazione, anche lui è un affermato scrittore e studioso, autore di *tenzi*<sup>2</sup>, *mashairi*<sup>3</sup> (apparsi su giornali e riviste) e numerosi saggi. Alcuni suoi saggi trattano del ruolo della poesia nella società, e del suo punto di vista sull'arte poetica. Così come Kezilahabi ha provato che la poesia in versi liberi può essere bella e concettualmente densa, Abdilatif Abdalla ha dimostrato che la poesia composta seguendo le forme prosodiche tradizionali ha ancora il suo fascino artistico e la capacità di trasmettere idee moderne e innovative. Ciò che è veramente importante, tuttavia, è il talento e lo spirito critico del poeta stesso.

I versi di Kezilahabi e Abdilatif Abdalla apparvero in un periodo di attivismo teso alla costruzione di una nuova società 'libera', dopo la colonizzazione occidentale in Tanzania e Kenya. Gli scontri e le tensioni sociali e politiche (etniche, di classe, economiche, partitiche, religiose) degli anni '60 e successivi emergono chiaramente nelle poesie di Kezilahabi e Abdalla contenute in questo libro.

Le tre raccolte poetiche di Kezilahabi riflettono le tre fasi storiche della Tanzania dopo l'Indipendenza. La prima fase, a partire dal 1961 fino al 1970, fu il periodo in cui si acclamava e celebrava l'Indipendenza, e al tempo stesso si rifletteva sul significato della stessa e sul tipo di società che si voleva costruire. Suddivisioni sociali e di classe erano già visibili, i leader al comando cominciarono ad arricchirsi mentre la maggioranza dei cittadini si impoveriva progressivamente e protestava. Si formò un ceto di persone chiamate *Wabenzi* (ossia i possessori di macchine di lusso, del tipo *Mercedes Benz*) le quali si giovavano delle risorse del paese e del governo senza curarsi delle condizioni di vita degli indigenti. Arrivati all'anno 1967, il partito al governo guidato da *Mwalimu J.K. Nyerere* si rese conto che il paese stava andando in una brutta direzione; c'era bisogno di una nuova visione e di un nuovo orientamento politico per far durare la coesione e l'amor di patria nel paese. Nel mese di febbraio di quello stesso anno venne proclamata la Dichiarazione di Arusha, che pose la Tanzania sul cammino in direzione dell'*Ujamaa*<sup>4</sup> (Socialismo africano) e del piano di Autosufficienza.



Mashairi ya Kezilahabi katika mikusanyo hii yanaunganisha falsafa ya mwandishi kuhusu maisha na uhalisi wa kisiasa na kiuchumi wa miaka thelathini ya uhuru. Katika shairi la “Jinamizi” (*Kichomi*, 1974, k. 1-2), watu “weusi na weupe” wamo mtumbwini na fimbo ndefu wakiwapiga samaki wanaojaribu kuinua vichwa juu ya maji ili kupata hewa. Baadaye mtumbwi unashambuliwa na mamba wenye meno makali na kupasuka, na samaki walio majini wanashangilia kwa kupata uhuru. Lakini wakati zahama hiyo ikitokea kuna majitu yanashuhudia na kuchekelea kwa mbali. Na mwandishi anatuambia:

Halafu nilifikiria Afrika  
Na siasa kwa ujumla  
- Mafuvu!

Hapa kuna ushirika wa weusi na weupe wanaoshirikiana kuwakandamiza wanyonge huku ‘majitu’ (wakoloni walio mbali?) yakicheka na kushangilia! Hali kama hii ya ukatili tunaiona katika shairi la “Tunatazamana” (*Kichomi*, 1974, k. 65-66) ambamo chungu kilichoko mekoni (Nchi?) kinachemka kwa moto wa kuni zilizokaushwa na jua la mkoloni; maji yanapochemka chungu kinavurugika kwa ‘mapinduzi’ na inabidi Baba atie unga wa uganga majini ili kuyatuliza. Ni picha nzuri na halisi ya vurugu ya Afrika baada ya uhuru. Unga (wa uganga) unaweza kuwakilisha utamaduni halisi na ontolojia ya Kiafrika. Siasa hizi za migongano ya baada ya uhuru zinakejeliwa pia katika shairi la “Mafahali Wapigana” (*Kichomi*, 1974, uk. 5) ambapo yule anayeshindwa anakimbia na mshindi anaketi kwenye kichuguu. Mwandishi anasema:

Patulivu! Patulivu! Patulivu!  
Lakini! Lakini! Lakini!

Tashtiti hii inadokeza ukweli kuwa hali si shwari, hivyo:

Tujenge kichuguu  
Kama mchwa tuungane...

Le poesie di Kezilahabi qui raccolte uniscono la filosofia dello scrittore riguardo l'esistenza, e la realtà politica e l'economica di trent'anni d'indipendenza. Nella poesia "Jinamizi" ("Incubo", *Kichomi*, 1974, pag. 1), persone "nere e bianche" si trovano in una barca e con un lungo bastone colpiscono i pesci che provano a sollevare la testa dall'acqua per prendere aria. In seguito, la barca viene attaccata da cocodrilli dai denti affilati e fatta a pezzi, e i pesci nell'acqua festeggiano per la ritrovata libertà. Ma durante il parapiglia, dei giganti stanno a guardare da lontano e ridono di loro. E il poeta ci dice:

Africa quindi pensai  
e politica  
- Teschi!

Vediamo qui un'associazione di neri e bianchi che collaborano nell'opprimere gli umili, mentre dei 'giganti' (i colonizzatori lontani?) ridono e festeggiano! Una condizione altrettanto crudele è esposta nella poesia "Tunatazamana" ("Ci guardiamo a vicenda", *Kichomi*, 1974, pagg. 65-66), dove una pentola di coccio che sta sul fuoco (il paese?) ribolle per il calore causato dalla legna asciugata dal sole del colonizzatore; quando l'acqua bolle, la pentola si agita a causa della 'rivoluzione', e occorre che il Padre versi della medicina tradizionale in polvere affinché l'acqua si calmi. È un'immagine bella e veritiera del caos in Africa dopo le indipendenze. La polvere medicinale (tradizionale) può rappresentare la cultura genuina e l'ontologia africana. Le politiche contraddittorie della post-indipendenza sono derise anche nella poesia "Mafahali Wapigana" ("Tori in combattimento", *Kichomi*, 1974, pag. 5)), dove colui che è sconfitto fugge via e il vincitore si siede su un nido di termiti. L'autore dice:

Quieto! Quieto! Quieto!  
Ma! Ma! Ma!

Questa satira suggerisce che in verità lo stato delle cose non è affatto tranquillo, per cui:

Costruiamo la colonia  
come termiti uniamoci

Kichuguu katika shairi hili ni ishara ya umoja na mshikamano, na katika utamaduni wa eneo la Maziwa Makuu ni ishara ya utawala, miviga na mizimu.

Kezilahabi ni mshairi wa kifalsafa. Tulipokuwa wanafunzi wake Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (1972-75), alizoea kutuuliza kama washairi wa Kiswahili tuliokuwa tukiwasoma walikuwa na falsafa yao iliyowaongoza au walitunga tu mashairi kulingana na mahitaji ya kupita ya wakati huo. Tulijadili sana hoja hiyo na kuona kuwa washairi wengi wa Kiswahili, isipokuwa labda Shaaban Robert na Muyaka, hawakuonesha kuwa na falsafa fulani maalumu. Mshairi Kezilahabi ni tofauti. Maudhui yake, pamoja na yale ya kisiasa, yanafumbatwa ndani ya falsafa. Falsafa ya Kezilahabi inachanganya mawazo ya Kimagharibi na ontolojia badilifu ya Mwafrika mwenyewe, na kujumuisha mapambano ya Mwafrika dhidi ya mfumo wa kijamii na kiuchumi wa ki-Magharibi wa kibepari unaomkandamiza, kwa ajili ya ukombozi wa kweli na mustakabali bora. Hivyo tofauti na utamauko (udhanaishi) wa Kimagharibi, utamauko wa Kezilahabi hauishii katika kukata tamaa tu, kuona kuwa Maisha hayana maana, bali unatafuta mabadiliko chanya ya mtu na jamii yaliyojikita katika misingi ya utu na ontolojia ya Mwafrika.

Katika mkusanyo wake wa kwanza wa *Kichomi*, Kezilahabi anatafakari suala la kifalsafa la Maisha na maana yake, na dalili za mtazamo wa utamauko (*existentialism*) zinajitokeza waziwazi, mathalan katika tungo za “Dhamira Yangu” (*Kichomi*, 1974, uk. 36) na “Fungueni Mlango” (*Kichomi*, 1974, uk. 23). Kezilahabi analitazama suala la maisha kama kipindi cha mateso (*kichomi*) yanayoambatana na msako wa ukweli na uhuru. Msako wa ukweli hauna mwisho, maana kufikiri hakuna mwisho (Kama kufikiri kumekwisha/Kuishi kungaliko? – “Kuishi”, *Karibu Ndani*, 1988, uk. 9). Maana ya Maisha imo katika kuutafuta ukweli unaomkomboa mwanadamu. Kisiasa, Kezilahabi anaiangalia hali ya Tanzania na Afrika kiupembuzi, na kubainisha mikinzano ya kijamii na usaliti wa viongozi na wasomi kwa wananchi ambao umeanza kujitokeza. Shairi lake la “Fasihi” (*Kichomi*, 1974, uk. 14) linadhihirisha nia yake ya kusema ukweli hata kama ni mchungu; linatabiri kuwa siku moja wenye nacho watampinga na kumkataa (mshairi), lakini wakifanya hivyo “msingi wao wa utamaduni watakuwa wameutupa.” Katika shairi hili

Il nido di termiti in questa poesia è simbolo di unione e solidarietà, e nella cultura della regione dei Grandi Laghi è un simbolo legato all'autorità, ai riti tradizionali e agli spiriti degli antenati.

Kezilahabi è un poeta filosofo. Quando eravamo suoi studenti all'Università di Dar es Salaam (1972-75), soleva chiederci se i poeti swahili che stavamo leggendo avessero una loro filosofia che li guidava, oppure componessero le poesie soltanto in base a necessità momentanee e transitorie. Discutemmo molto su questo punto e concludemmo che molti poeti swahili, a eccezione forse di Shaaban Robert e Muyaka, non mostravano di possedere una particolare filosofia. Il poeta Kezilahabi è differente. I suoi contenuti, insieme a quelli di natura politica, sono immersi nella filosofia. La filosofia di Kezilahabi amalgama concetti occidentali e l'ontologia in divenire dell'Africano, e si unisce alle battaglie dell'Africano contro il sistema socio-economico capitalistico occidentale che lo opprime, al fine di una vera liberazione e di un futuro migliore. Perciò, diversamente dall'esistenzialismo occidentale, l'esistenzialismo di Kezilahabi non conduce soltanto alla disperazione, al vedere che l'Esistenza non ha alcun senso, ma alla ricerca di cambiamenti positivi dell'essere umano e della società, fondati sull'umanità<sup>5</sup> e l'ontologia dell'Africano.

Nella sua prima raccolta poetica, *Kichomi*, Kezilahabi medita sulla questione filosofica dell'Esistenza e sul suo significato, e tracce della visione esistenzialista vi appaiono chiaramente, come ad esempio nelle poesie "Dhamira Yangu" (La mia coscienza 1974, 36) e "Fungueni Mlango" ("Aprite la porta", *Kichomi*, 1974, pag. 23). Kezilahabi guarda all'esistenza come un periodo di dolore dilaniante (*kichomi*) che va di pari passo con la ricerca della verità e della libertà. La ricerca della verità non ha fine, poiché il riflettere non ha fine (Se terminato è il pensare/persiste il vivere? – "Kuishi", "Vivere", *Karibu Ndani*, 1988, pag. 9). Il senso dell'Esistenza si trova nella ricerca della verità che porta alla liberazione dell'essere umano. Dal punto di vista politico, Kezilahabi vaglia al setaccio la condizione della Tanzania e dell'Africa, e evidenzia i conflitti sociali e il tradimento di leader e intellettuali nei confronti dei cittadini, che cominciava a manifestarsi. La sua poesia "Fasihi" ("Letteratura", *Kichomi*, 1974, pag. 14) mette in chiaro la sua intenzione di dire la verità anche se dolorosa; predice che un giorno i suoi connazionali lo

tunaona namna Kezilahabi anavyounganisha suala la ushairi (hususani ushairi “mpya” wa masivina alioshiriki kuuanzisha) na *ujadi* halisi wa Mwafrika na ukweli wa maisha na siasa.

Kipindi cha pili nchini Tanzania ni cha takriban miaka ya 1970 hadi 1985 ambapo sera za Ujamaa zilikuwa zikitekelezwa. Mfumo wa uchumi ulibadilishwa, njia kuu za uchumi zilitaifishwa, vijiji vya Ujamaa vilianzishwa na Tanzania ilianza kutolewa mfano kama nchi ya Kiafrika yenye mwelekeo wenye matumaini.

Kezilahabi anauona upande mzuri wa mabadiliko haya, lakini pia anauona udhaifu wake na ufupi wake kiwakati. Falsafa yake haimruhusu kukubali kuwa sasa tumefikia ‘nchi ya ahadi’ na mambo yatakuwa mema. Hivyo badala ya kushangilia Ujamaa, anausaili na kutushawishi tuutafakari zaidi, mbali na kuonyesha dosari za utekelezaji wa sera hiyo. Hatimaye, kufikia miaka ya 1980, anaweza kutabiri kifo cha Ujamaa (*Karibu Ndani*, 1988, uk. 19):

Waanzilishi wametupa chini  
Mawe ya Amri na Miiko kwa hasira  
Na kupanda magari mapya yatupofushayo macho.  
Sisi kwa sisi tukilana, safari lazima iendelee?

Ishara hii ya Musa wa Biblia na “Amri Kumi za Mungu” inawakilisha vizuri usaliti unaotokea. Katika shairi la “Azimio” (*Karibu Ndani*, 1988, uk. 27) Kezilahabi anaandika tahalili ya Azimio:

Azimio sasa ni mabaki ya chakula  
Kwenye sharubu za bepari  
Kalamu inayovuja  
Katika mfuko wa mwanafunzi  
Vumbi zito  
Baada ya ng’ombe kupita...  
Kilichosalia sasa  
Ni punje za ulezi  
Zilizosambazwa jangwani  
Na mpandaji kipofu.

Haya yaliandikwa kabla ya Azimio la Zanzibar la mwaka 1992 lililoutupilia mbali sera za Ujamaa. Pamoja na kukiri kuanguka kwa Ujamaa, Kezilahabi bado anaonesha matumaini katika

contesteranno e lo rifiuteranno (il poeta), ma così facendo “della cultura loro il fondamento/ avranno gettato”. Nella poesia vediamo il modo in cui Kezilahabi unisce la questione della poesia (in particolare della poesia “nuova” senza rima, al cui avvio egli contribuì), di cosa sia la tradizione africana e della verità esistenziale e politica.

La seconda fase storica della Tanzania va all'incirca dal 1970 al 1985, quando le politiche dell'*Ujamaa* vennero messe in atto. Il sistema economico venne modificato, l'apparato economico venne nazionalizzato, i villaggi socialisti vennero avviati e la Tanzania cominciò ad esser guardata come a un modello di paese africano che procedeva in modo incoraggiante.

Kezilahabi vide l'aspetto positivo di questi mutamenti, ma ne vide anche i punti deboli e la miopia. La sua filosofia non gli consentiva di accettare che fossimo giunti alla 'terra promessa' e tutto sarebbe andato bene. Perciò, piuttosto che festeggiare l'*Ujamaa*, la interrogò e ci esortò a continuare a riflettere criticamente, oltre a mostrare i difetti nell'implementazione delle politiche socialiste. Infine, durante gli anni '80, predisse la fine dell'*Ujamaa* (*Karibu Ndani*, 1988, pag. 19):

Gli iniziatori hanno scaraventato  
pietre del Comando e dei Tabù con rabbia  
e sono andati con nuove auto che ci accecano.  
Se ci mangiamo a vicenda, il viaggio deve continuare?

Questo riferimento a Mosè e ai Dieci Comandamenti rappresenta bene il tradimento avvenuto. Nella poesia “Azimio” (“Dichiarazione”; *Karibu Ndani*, 1988, pag. 27), Kezilahabi scrive un necrologio per la Dichiarazione (di Arusha):

La dichiarazione è il resto del cibo  
Sui baffi del capitalista  
rotta è la penna  
nella tasca dello studente  
Coltre di polvere dopo il passaggio della vacca [...]  
ciò che resta  
semi di miglio  
sparsi nel deserto  
da un seminatore cieco.

uwezo wa Umma wa kuyabadilisha mambo (*Karibu Ndani*, 1988, uk. 31):

Kokeni mioto mashujaa wa uonevu tuwabanike  
Kamwe hapatakuwa na kilio wala matanga  
Bali hoi hoi za ushindi na madaraka kwa umma.

Tanzia ya maisha ya Mwafrika kisiasa na kifalsafa inaelezwa vizuri katika mkusanyo wa *Karibu Ndani*. Tunaoneshwa kuwa pamoja na kwamba binadamu hufanya mambo bila kujua hakika ya kesho, bila kujua hatima yake; lakini bado ni muhimu kuendelea ‘kumsaka paa gizani’ (*Nagona*) kwa kuwa hakuna mwisho wa kutafuta ukweli.

Katika mkusanyo wa tatu, *Dhifa*, Kezilahabi anatupeleka katika ulimwengu wa ufisadi na utandawazi uliofuatia maziko ya Azimio. Baada ya kuutelekeza Ujamaa na kubinafsisha mali ya Umma, sasa tabaka tawala linafanya dhifa (tafrija) ili kutafuna mali waliyoiiba (“Dhifa”, *Dhifa*, 2008, uk. 22):

Ni chakula cha mchana.  
Walanchi wameshafika:  
Wazungu, Wahindi, Waarabu  
Weshateka sehemu zao.  
Chakula ki mezani.  
Ni dhifa....

Tashtiti ya mageuzi na mabadiliko yaliyojaa kejeli tunaiona katika shairi la “Nani Kaua” (*Dhifa*, 2008, uk. 24) ambapo dhana zinazokanganya na kutisha watu zinageuzwa kichekesho.

Kezilahabi haizungumzii Tanzania tu; anaizungumzia Afrika, ulimwengu mzima. Katika “Maendeleo si Ndwele” (*Dhifa*, 2008, uk. 47) tunaambiwa “Baba atoka chumbani na bunduki akiyumba/ akiimba wimbo wa Taifa la Afrika.” Lakini Afrika hii “Maendeleo yameipiga chenga” na “Mbele ramani ya Afrika imenasa mtini” (shairi la “Mtakaso”, *Dhifa*, 2008, uk. 19).

Lakini haishii hapo, bado anaturudisha katika falsafa ya kuishi, ya kuwapo na kuwa (shairi la “Wakati Fulani”, *Dhifa*, 2008, uk. 15):

Wakati fulani utafika,  
Hadi wakati wawa kifo.

Questi versi vennero scritti ben prima che la Dichiarazione di Zanzibar del 1992 abbandonasse definitivamente l'*Ujamaa*. Insieme ad affermare la caduta dell'*Ujamaa*, Kezilahabi mostra ancora qualche speranza nella capacità del Popolo di cambiare le cose (*Karibu Ndani*, 1988, pag. 31):

Mettete sul fuoco gli eroi dell'oppressione affumichiamoli  
non ci sarà nessun lamento funebre né lutto  
ma hip hip urrà della vittoria e autorità per il popolo.

L'annuncio funebre è cifra dell'esistenza tragica dell'Africano dal punto di vista politico e filosofico, ed è illustrato bene nella raccolta *Karibu Ndani*. Ci viene mostrato che assieme al fatto che l'essere umano suole fare le cose senza avere la certezza del domani, senza sapere il suo destino, è comunque importante continuare a 'cercare la gazzella nell'oscurità' (*Nagona*) poiché non vi è termine alla ricerca della verità.

Nella sua terza raccolta poetica, *Dhifa*, Kezilahabi ci conduce in un mondo di corruzione e globalizzazione successivo alla sepoltura della Dichiarazione [di Arusha]. Dopo aver abbandonato l'*Ujamaa* e privatizzato i beni della Nazione, ora le classi governanti fanno un banchetto per masticare le ricchezze che hanno derubato ("Dhifa", "Il banchetto", *Dhifa*, 2008, pag. 22):

Per il pranzo.  
Già giunti i commensali:  
occidentali, indiani, arabi  
hanno già preso il loro posto.  
Il pasto è a tavola.  
è un banchetto

La satira nei confronti delle trasformazioni e degli sfacciati cambiamenti emerge anche nella poesia "Nani Kaua" ("Chi ha ucciso", *Dhifa*, 2008, pag. 24) in cui le idee che disorientano e minacciano la gente vengono trasformate in una farsa.

Kezilahabi non parla solo della Tanzania; parla dell'Africa, del mondo intero. In "Maendeleo si Ndwele" ("Il progresso non è una malattia", *Dhifa*, 2008, pag. 47) leggiamo "Il Padre esce barcollante dalla stanza con un fucile in mano/cantando l'inno nazionale dell'Africa". Ma l'Africa "Ha schivato il progresso" e "Più in là la mappa dell'Africa è attaccata all'albero" ("Mtakaso", "Purificazione", *Dhifa*, 2008, pag. 19).



Kutojua ni kujua.  
Kuishi ni kufa.

Na licha ya madhila tunayopashwa na watesi wetu (watawala, wanyonyaji), mwandishi anaona bado kuna matumaini na hatupaswi kukata tamaa (“Njia Tuliyoipitishwa”, *Dhifa*, uk. 3; msisitizo ni wangu):

Ingawa hatuna machozi ya moto  
Yatakayofuta aibu hii tukufu  
Bendera ya haki itapepea daima  
Daima *tutakuwa* na *kuwako*.  
Mbele ya umoja thabiti  
Milima na vichuguu hulala.

Vipindi vitatu vinavyowakilishwa na mikusanyo mitatu za Kezilahabi havijitokezi katika ushairi wa Abdilatif Abdalla kwa kuwa mashairi yake yanatoka katika diwani moja tu iliyochapishwa mwaka 1973. Hata hivyo, kuna mshabaha kati ya mkusanyo wa kwanza wa Kezilahabi na ule wa Abdilatif Abdalla. Diwani ya Abdilatif Abdalla inaitwa *Sauti ya Dhiki* na mkusanyo wa Kezilahabi unaitwa *Kichomi*. Majina hayo yanadokeza hali fulani ya machungu na mateso. Mateso ya Kezilahabi ni ya moyoni na nafsi, na ya Abdilatif Abdalla ni ya nafsi na mwili. Aliyatunga mashairi yake akiwa gerezani nchini Kenya. Shairi la Abdilatif Abdalla la “N’Shishiyelo ni Lilo” (*Sauti ya dhiki*, 1974, uk. 1) linabainisha pande mbili zinazopambana na kuisisitiza msimamo wake wa kuendelea kutetea kweli:

Kweli naliwaambiya, wakuu wa nti hini  
Haeleza moya moya, kwa wanati wa ntini  
Kuhusu walofanyiya, upande wa Upinzani  
Sasa kuwamo tabuni, nalipwa kwa hiyo kweli (ubeti wa 5)

Wangi washasumbuliwa, waneni wa kweli hiyo  
Na wangi washauliwa, kwa kutobadili nyoyo  
Na mimi nimeradhiwa, ku’yandama sera hiyo  
“Tafuawata zao nyayo, n’shishiyelo ni lilo... (ubeti wa 19)

Ngonjera ya “Mnazi: Vuta N’Kuvute” (*Sauti ya dhiki*, 1974, uk. 17) inasawiri vizuri mgawanyiko na mkinzano wa kitabaka uliokuwamo

E non finisce qua, ancora ci fa tornare alla filosofia del vivere, dell'essere e dell'essere ("Wakati Fulani", "Un certo tempo", *Dhifa*, 2008, pag. 15):

arriverà un tempo,  
finché il tempo sia morte.  
Non sapere è sapere.  
Vivere è morire.

Ma nonostante le sofferenze procurateci dai nostri persecutori (governanti, sfruttatori), lo scrittore ritiene che vi siano ancora speranze e che non bisogna scoraggiarsi ("Njia Tulyopitishwa", "La strada per cui siamo passati"; *Dhifa*, 2008, pag. 3; corsivo mio):

Sebbene non abbiamo calde lacrime  
ciò che ci cancella questa santa vergogna  
la bandiera dei diritti sventolerà sempre  
sempre avremo esistenza.  
Di fronte alla ferma unità  
montagne e formichieri dormono.

Le tre fasi storiche [della post-indipendenza] che sono rappresentate dalle tre raccolte poetiche di Kezilahabi non appaiono nella poesie di Abdilatif Abdalla poiché esse provengono dalla sua unica raccolta poetica, pubblicata nel 1973. Detto questo, vi sono delle rassomiglianze tra la prima raccolta poetica di Kezilahabi e quella di Abdilatif Abdalla. La raccolta poetica di Abdilatif Abdalla si intitola *Sauti ya Dhiki* (La voce dell'agonia) e quella di Kezilahabi *Kichomi* (Dolore dilaniante). Questi titoli indicano una certa condizione di dolore e tormenti. I tormenti di Kezilahabi sono del cuore e dello spirito, quelli di Abdilatif Abdalla dello spirito e del corpo. Egli ha composto le sue poesie mentre era rinchiuso in carcere in Kenya. La poesia di Abdilatif Abdalla "N'Shishiyelo ni Lilo" ("A questo io m'afferro"; *Sauti ya dhiki*, 1974, pag. 1) mette in chiaro le due parti in gioco e evidenzia la sua posizione, ossia il continuare a difendere la verità:

La verità ho detto, ai capi della nazione  
Ogni cosa ho spiegato, al cittadino comune  
Su quello che hanno fatto, all'ala d'opposizione  
Ora c'è complicazione, mi fan pagar la verità (strofa 5)

nchini Kenya miaka ya 1960 na 1970. Leo, mwaka 2017, mgawanyiko na mkinzano huo bado upo, au labda umeongezeka. Yaelekea safari ya kwenda kwenye haki na usawa ni ndefu; miaka hamsini haitoshi.

Hata hivyo, Abdilatif Abdalla hajakata tamaa; anaona kuwa hatimaye ushindi utapatikana. Falsafa ya Abdilatif Abdalla katika mashairi haya, kama ilivyo falsafa ya kisiasa ya Kezilahabi tuliyoijadili, inaunganisha dhana za umoja na ukombozi wa wanyonge (harakati za kitabaka), umajumui wa Kiafrika (shairi la “Mamaetu Afrika”, *Sauti ya dhiki*, 1974, uk. 36), na uhakika wa mabadiliko na ushindi. Mshairi ana matumaini kuwa kila liwalo lina mwisho, na hata mateso yanayomkumba sasa, na yanayowakabili Wakenya, hatimaye yatakwishwa. Na katika shairi la “Mamba” (*Sauti ya dhiki*, 1974, uk. 10) tunaambiwa kwamba huyo mamba mkandamizaji hatadumu:

Akumbuke, siku yake ikifika  
Roho yake, ajuwe itamtoka  
Nguvu zake, kikomoche zitafika

Afahamu, mtu hajuwi la kesho  
Hatadumu, angatumiya vitisho  
Maadamu, lenye mwanzo lina mwisho...

Je, leo, takriban miaka arobaini baadaye, huyo Mamba bado yupo? Jibu ni kwamba yungalipo, lakini si kwa takaburi kama wakati ule. Leo analazimika kushindana na ‘mamba’ wengine baada ya mageuzi ya vyama vingi nchini Kenya, na yumkini siku zake zinakaribia ukomo.

Je, ni mamboganiyanawaunganisha Abdilatif Abdalla na Kezilahabi? Ni mengi, lakini hapa tutagusia mawili tu. Kwanza ni muktadha wa tungo zao, hasa ule wa miaka ya 1960 (japo hata sasa tungo za Abdilatif Abdalla bado zinaakisi kwa kiasi fulani hali ya sasa ya Kenya, maana mfumo wa kiuchumi haujabadilika). Wote wawili wanautafakari uhalisi wa matatizo ya Afrika Mashariki na kujaribu kupata majibu. Pili, falsafa. Wote wawili wana falsafa ya mabadiliko; wanaamini kuwa hali haiwezi kuendelea kama ilivyo milele. Na wote wawili wanaona kuwa mabadiliko chanya ni yale yanayomkomboa mwanadamu. Kwa Kezilahabi, kisichobadilika ni msako wa ukweli, na kwa Abdilatif Abdalla ni msimamo wake wa utetezi wa wanyonge, ambao pia ni aina ya msako wa ukweli. Kadhalika, wote wawili wana falsafa ya utetezi wa

Molti hanno attaccato, che il vero avean detto  
Molti hanno ammazzato, perch'idea non han cambiato  
Ed io sono appagato, di accoglier questo fato  
Seguirò l'orme da dietro, a questo io m'afferro (strofa 19)

La *ngonjera*<sup>6</sup> “Mnazi: Vuta N’Kuvute” (“Palma da cocco: botta e risposta”; *Sauti ya dhiki*, 1974, pag. 17) riflette bene le suddivisioni e i conflitti sociali che esistevano in Kenya negli anni ’60 e ’70. Oggi, nel 2017, disparità e conflitti ancora esistono, anzi forse sono aumentati. Pare che il cammino verso la giustizia e l’eguaglianza sia molto lungo; cinquant’anni non bastano.

Ad ogni modo, Abdilatif Abdalla non perde la speranza; ritiene che alla fine vincerà. Il pensiero di Abdilatif Abdalla in queste poesie, così come il pensiero politico di Kezilahabi che abbiamo appena discusso, collega il concetto di unità e liberazione degli oppressi (lotta di classe), il Panafricanismo (nella poesia “Mamaetu Afrika”, “Nostra Madre Africa”, *Sauti ya dhiki*, 1974, pag. 36), e la certezza del cambiamento e della vittoria. Il poeta ha fiducia poiché ogni cosa ha una fine, e anche i tormenti che lo affliggono, e che devono affrontare i Keniotti, infine termineranno. Nella poesia “Mamba” (“Il coccodrillo”; *Sauti ya dhiki*, 1974, pag. 10) il poeta dice che il coccodrillo oppressore non durerà:

Sia memore, il suo giorno arriverà  
’l suo essere, sappia che s’allontanerà  
Del potere, il termine arriverà

Colga bene, l’omo il domani non sa  
Non rimane, se le minacce userà  
La ragione, è che l’inizio fine ha

E oggi, quasi quarant’anni dopo, il Coccodrillo c’è ancora? La risposta è che c’è ancora, ma non con la stessa superbia di quel tempo. Oggi è costretto a competere con altri ‘coccodrilli’ dopo l’introduzione del multipartitismo in Kenya, e forse ci avviciniamo alla fine dei suoi giorni.

Quali sono gli aspetti che accomunano Abdilatif Abdalla e Kezilahabi? Sono molti, ma qui ne toccheremo solo due. Il primo è il contesto in cui sono nati i loro componimenti, in particolare quello della post-indipendenza (sebbene le poesie di Abdilatif Abdalla riflettano ancora la

wanyonge na umajumui wa Kiafrika (kama ambavyo tumeonesha hapo juu).

Kisanaa, washairi hawa wanatumia lahaja tofauti za Kiswahili: Kezilahabi anatumia Kiswahili Sanifu chenye ladha ya Kikerewe wakati Abdilatif Abdalla anatumia Kimvita asilia. Kezilahabi anatumia lugha rahisi ya mazungumzo lakini iliyosheheni tamathali, hasa sitiari, ishara na udokezi; anaandika mashairi magumu kwa lugha rahisi. Abdalla anaandika kwa lugha rahisi ya Kimvita lakini yenye wizani na utamu sikioni. Kwa hakika Kimvita kinanogesha ushairi wake. Mbinu za kale za utunzi zinatumiwa kwa usahihi na ustadi mkubwa. Mbali na tofauti hii ya lahaja na arudhi, washairi hawa wanashabihiana kwa kutumia jazanda na ishara kwa wingi katika tungo zao. Kezilahabi aliwahi kuandika kuwa jazanda na ishara ndio moyo wa ushairi wa jadi wa Kiafrika. Abdilatif Abdalla anatumia picha za mamba, jimbi, mtu aliye mnazini, mtoto aliye tumboni, Mama (Afrika), na nyinginezo kuwasilisha maudhui yake. Kezilahabi anatumia ishara za kijijini, majini (mamba na mashua), mafuvu, damu na mauti, pande za dunia (mashariki, magharibi), nyumba, milango na madirisha, kelele na kimya, mimea na mbegu, visasili na visakale, ngoma, duara, n.k. kuumba maudhui yake.

Pamoja na mshabaha huo, washairi hawa wawili wanatofautiana kifani. Abdilatif Abdalla anatumia maumbo ya kimapokeo yenye urari mzuri wa vina na mizani, wakati Kezilahabi anakataa kufungwa na kanuni za kijadi na hivyo kuupeleka msako wa uhuru na ukweli hadi katika medani ya ushairi. Ni vigumu kwa mfasiri katika lugha nyingine kuwasilisha uhalisi wa sanaa ya Kezilahabi au Abdilatif Abdalla. Maana, japo ushairi wa Kezilahabi hauna urari wa vina na mizani, lakini una urari wa vipashio na mpangilio wa lugha na uteuzi wa maneno na dhana ambao si rahisi kuutia katika lugha nyingine. Ushairi wa Abdilatif Abdalla unatumia mbinu za kishairi za kijadi kama vina na takriri ambazo bila shaka hazitafsiriki katika lugha nyingi. Mfano mzuri ni takriri ya sauti ya **k** na kina cha **ku** (pia *n*) katika shairi la “Kuno Kunena” (*Sauti ya dhiki*, 1974, uk. 23):

**Kana na huku kunena, kunenwa hakutakiwi**  
**Kuna wanakokuona, kunena kwamba si kuwi**

condizione contemporanea del Kenya, poiché il sistema economico non è granchè cambiato). Entrambi hanno scandagliato la realtà dei problemi dell'Africa orientale e tentato di dare delle risposte. Entrambi hanno una concezione fondata sul dinamismo; credono che le cose non possano restare così come sono in eterno. Ed entrambi ritengono che i mutamenti positivi siano quelli che liberano l'essere umano. Per Kezilahabi, ciò che non cambia è la ricerca della verità, per Abdilatif Abdalla è la sua posizione in difesa degli oppressi, che a ben vedere è anch'essa una ricerca della verità. Inoltre, entrambi mettono al centro del loro pensiero la difesa degli oppressi e del Panafricanismo (come abbiamo detto sopra).

Dal punto di vista artistico, questi due poeti adoperano due varietà diverse di swahili: Kezilahabi utilizza lo swahili standard con influenze del Kikerewe<sup>7</sup>, mentre Abdilatif Abdalla scrive in dialetto Kimvita<sup>8</sup>. Kezilahabi utilizza il linguaggio semplice delle conversazioni quotidiane, ma ricco di figure retoriche, specialmente metafore, simbolismi e allusioni; scrive delle poesie difficili con un linguaggio semplice. Abdalla scrive in dialetto Kimvita utilizzando un linguaggio essenziale, ma denso di significati e molto musicale. Senza dubbio il dialetto Kimvita rende piacevole la sua poesia. Gli schemi prosodici tramandati nel tempo [lungo la costa swahili] vengono utilizzati con grande sapienza e abilità. A parte le differenze che riguardano la varietà della lingua e la prosodia, questi poeti si assomigliano per quanto concerne l'utilizzo abbondante del linguaggio figurato e dei simbolismi nelle loro poesie. Kezilahabi ha scritto che il linguaggio figurato e i simbolismi sono l'essenza della poesia tradizionale africana. Abdilatif Abdalla usa immagini di coccodrilli, galli, di una persona in cima ad una palma di cocco, di un bambino nel ventre materno, della Madre (Africa), e tante altre per veicolare i suoi contenuti poetici. Kezilahabi utilizza il simbolismo del villaggio, dell'acqua (coccodrilli e barche/canoe), dei teschi, del sangue e della morte, delle regioni della terra (oriente, occidente), della casa, delle finestre e delle porte, delle urla e del silenzio, delle piante e dei semi, dei miti e delle leggende, delle *ngoma*<sup>9</sup>, del cerchio, etc. per dar forma ai suoi contenuti.

Assieme a queste rassomiglianze, vi sono anche delle differenze stilistiche tra i due poeti. Abdilatif Abdalla utilizza le forme poetiche tradizionali basate sulla regolarità metrica e della rima, mentre

**Kunena wa***kikuona*, **kuku***ita* **kawa***kawi*  
**Kunena** *kana* **kwanu***ka*, **niku***kome* **kuku***nena*?

Ni kazi ngumu kutafsiri sauti hizo katika Kiitaliano au lugha nyingineyo!

Nimalizie Utangulizi huu kwa kurudia ahadi yangu niliyoitoa mwanzoni kuwa sikusudii kufanya uhakiki au uchambuzi wa mkusanyo huu; azma yangu ilikuwa ni kueleza machache ninayoyafahamu kuhusu washairi wetu, Maprofesa E. Kezilahabi na A. Abdalla, na kazi zao, ili kuwapa mweka wa usuli wasomaji wa mashairi haya, hasa wale wasiokuwa na taarifa za kutosha kuhusu muktadha wa kifikra, kijamii na kisiasa wa tungo hizi. Natumaini azma hiyo nimeitimiza. Namalizia Utangulizi huu kwa kuwashukuru waandaaji wa kitabu hiki kwa kuona umuhimu wa kukiandaa na kukichapisha katika lugha ya Kiitaliano; matumaini yangu ni kwamba chapisho hili halitabakia katika Kiitaliano tu, bali litafasiriwa na kuchapishwa katika lugha nyingi nyingine za dunia.

M. M. Mulokozi

*Profesa – Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*

*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

*5/4/2017*

Kezilahabi rifiuta di essere bloccato dalle regole tradizionali e così ha portato la ricerca della libertà e della verità fino al campo della poesia. È difficile per il traduttore rendere in un'altra lingua l'essenza dell'arte di Kezilahabi o Abdilatif Abdalla. Infatti, sebbene la poesia di Kezilahabi non presenti regolarità prosodica (metro e rima), possiede tuttavia una disposizione dei costituenti, un'architettura della lingua e una scelta delle parole e dei concetti che non sono facili da tradurre. La poesia di Abdilatif Abdalla si basa sulle tecniche poetiche tradizionali come la rima, le ripetizioni e allitterazioni, queste ultime sicuramente intraducibili in molte lingue. Un buon esempio è la ripetizione del suono **k** (anche della **n**) e della sillaba **ku** nella poesia "Kuno Kunena" ("Questo parlare"; *Sauti ya dhiki*, 1974, pag. 23):

**K**ana na huku **kun**ena, **kun**enwa haku**t**akiwi  
**K**una wana**k**okuona, **kun**ena **k**wamba si **ku**wi  
**Kun**ena wa**k**ikuona, **kuku**ita **k**awa**k**awi  
**Kun**ena **k**ana **k**wanu**k**a, **niku**kome **kuku**nena?<sup>10</sup>

È molto difficile rendere questi suoni in italiano o in qualsiasi altra lingua!

Vorrei concludere questa introduzione ritornando alla promessa fatta all'inizio, cioè di non fare un'analisi critica delle poesie raccolte in questo libro; la mia intenzione era di spiegare alcune delle cose che conosco sui nostri poeti, i professori E. Kezilahabi e A. Abdalla, e sulla loro opera, al fine di fornire utili informazioni ai lettori delle poesie, specie quelli che conoscono poco il contesto intellettuale, sociale e politico dei componimenti. Spero di aver portato a compimento il mio proposito. Concludo l'introduzione ringraziando i curatori del libro per aver colto l'importanza di lavorare a questa raccolta e per averla pubblicata in italiano; il mio augurio è che questa pubblicazione non rimanga solo in italiano, ma venga tradotta e pubblicata anche in altre lingue del mondo.

M. M. Mulokozi  
*Professore – Dipartimento di Studi Swahili*  
*Università di Dar es Salaam*  
5/4/2017



## Note

<sup>1</sup> *Ndt*: *mwalimu* (maestro, insegnante) è un titolo di rispetto in swahili.

<sup>2</sup> *Ndt*: i *tenzi* o *tendi* (singolare *utenzi/utendi*) sono componimenti, generalmente piuttosto lunghi, costituiti da strofe di quattro versi — o, secondo alcuni, due versi con cesura centrale — con otto sillabe per rigo ed uno schema metrico del tipo ‘aaab’. Questa forma è spesso utilizzata nella letteratura swahili per la versificazione di narrazioni a sfondo storico o religioso (cfr. Alamin Mazrui, *Swahili beyond the Boundaries. Literature, Language, and Identity*. Athens, Ohio University Press, 2007: 17).

<sup>3</sup> *Ndt*: i *mashairi* (singolare *shairi*) sono poesie le cui strofe sono costituite da un ugual numero di versi (generalmente quattro) e da un ugual numero di sillabe per ogni verso (solitamente non più di sedici, divise al centro da una cesura). Lo schema metrico classico di ogni strofa è del tipo ‘ab/ab/ab/bx’, ma i poeti, soprattutto quelli contemporanei, tendono ad introdurre diverse varianti per quanto riguarda le rime dell’ultimo verso. Questo tipo di poesia è molto popolare in Africa orientale: i *mashairi* vengono regolarmente pubblicati sulla stampa swahili o letti/recitati durante programmi radiofonici in Tanzania e Kenya (cfr. Farouk Topan, “Modern Swahili Poetry”, *Bulletin of the School of Oriental and African Studies* 37,1974: 176).

<sup>4</sup> *Ndt*: *ujamaa* in swahili vuol dire parentela, fratellanza, senso di coesione tra i membri di una comunità. Nyerere utilizzò questo termine per trasmettere la sua concezione di socialismo africano: “*Ujamaa*, then, or familyhood, describes our socialism. It is opposed to capitalism, which seeks to build a happy society on the basis of the exploitation of man by man; and it is equally opposed to doctrinaire socialism which seeks to build its happy society on a philosophy of inevitable conflict between man and man.” In: J. K. Nyerere, *Freedom and Unity/Uhuru na Umoja*. Dar es Salaam, Oxford University Press, 1966:166.

<sup>5</sup> *Ndt*: la nozione swahili *utu*, tradotta solitamente con umanità, implica, a vari livelli, sia la rettitudine etica e la fideità, sia le buone azioni attraverso cui essa diviene esplicita (cfr. Kai Kresse, *Philosophising in Mombasa: Knowledge, Islam and Intellectual Practice on the Swahili Coast*, Edimburgh, Edinburgh University Press, 2007).


<sup>6</sup> La *ngonjera* è un genere di poesia dialogata e drammatizzata, originario di alcuni gruppi etnici del continente tanzaniano, che negli anni del socialismo venne modernizzato e adattato alla lingua e tradizione metrica swahili dal poeta Mathias Mnyampala. Cfr. Elena Bertocini Zúbková et al., *Outline of Swahili Literature*. Leiden, Brill, 2009: 233.

<sup>7</sup> *Ndt*: il *Kikerewe* è una lingua bantu parlata principalmente sull’isola di Ukerewe, nel lago Vittoria, in Tanzania.

<sup>8</sup> *Ndt*: il *Kimvita* è un dialetto primario swahili, parlato principalmente nella città di Mombasa, in Kenya.

<sup>9</sup> *Ndt*: *ngoma* è un termine swahili che significa letteralmente ‘tamburo’, ma che per sinecdoche è riferita alle performance in cui interagiscono musica, danza e canto, in occasione degli eventi rituali delle comunità. Cfr. Irene Brunotti, *Chake/Wete in Ng’ambo: Ngoma e costruzioni identitarie a Zanzibar in età contemporanea*. Tesi di dottorato, Università degli Studi di Napoli “L’Orientale”, Napoli, 2005, p. 14.

<sup>10</sup> Seppure questo parlare, non lo si può proferire/Taluni posson pensare, che male non sia il dire/E sentendo ‘sto parlare, venir a interloquire/Se il mio parlar vi puzza, dovrei smetter di parlare?



Euphrase Kezilahabi (kushoto/a sinistra) - Abdilatif Abdalla (kulia/a destra).  
Aprili/Aprile 1977, Mainz, Ujerumani/Germania.



Kutoka kushoto/da sinistra: Prof. Grohs, Euphrase Kezilahabi, Abdilatif Abdalla,  
Ebrahim Hussein. Aprili/Aprile 1977, Mainz, Jahnheinz Jahn Symposium.



Kutoka kushoto/ da sinistra: Abdilatif Abdalla, Euphrase Kezilahabi, Ebrahim Hussein, Thilo Schadeberg.  
Aprili/Aprile 1977, Mainz, Ujerumani/ Germania.



Abdilatif Abdalla na/e Euphrase Kezilahabi.  
Desemba/dicembre 1978, Chuo Kikuu cha/Università di Dar es Salaam,  
Tanzania.





**Tungo za A. Abdalla na tafsiri yao kwa Kiitaliano**

*ya F. Aiello*

**Poesie di A. Abdalla e traduzioni in italiano**

*di F. Aiello*

## **N'shishiyelo ni Lilo**

Nipulikiza ndu yangu, ninenayo usikiye  
Yaliyo moyoni mwangu, ningependa nikwambiye  
Ujuwe imani yangu, ambayo niishishiye  
Siiwati ingawaye, n'shishiyelo ni lilo

Walineni walimwengu, wa zama zilopisiye  
Kwamba kweli i utungu, kwa yule aambiwaye  
Nami haya ndugu yangu, sasa niyaaminiye  
Asojuwa nasikiye, apeleleze ajuwe

Kweli nnaifahamu, haipendwi aswilani  
Kwa mja hiyo ni sumu, mbaya iso kifani  
Mwenye kuitakalumu, hapendezi katwaani  
Sasa nshayaamini, ni kweli haya ni kweli

Kweli imenitongeya, kwa kuinena mwendani  
Wale nalowaambiya, wamenitiya dhikini  
Wameniona mbaya, kumshinda Firauni  
Kweli, sasa naamini, si wangi waipendao

Kweli naliwaambiya, wakuu wa nti hini  
Haeleza moya moya, kwa wanati wa ntini  
Kuhusu walofanyiya, upande wa Upinzani  
Sasa kuwamo tabuni, nalipwa kwa hiyo kweli

Kweli ilipowatoma, kama dasturi yake  
Wao wakaona vyema, afadhali wanishike  
Wanishike hima hima, hima ndani waniweke  
Ngomeni n'adhibike, nijute kusema kweli

## **A Questo io mi afferro**

Ascolta amico mio, quel che ti dico senti  
Ciò che è nel cuor mio, mi piacerebbe dirti  
Sappi che il credo mio, per cui stringo i denti  
Non mollo a tutt' i costi, a questo io mi afferro

Gli uomini dissero, in quel tempo passato  
Che il vero è amaro, a chi vien proferito  
Ed io o fratello caro, ora a ciò ho creduto  
Chi non sa presti ascolto, investighi per sapere

Il vero io bene lo so, non è amato affatto  
Per l'uomo è velenoso, orribile più di tutto  
Chi lo dice deciso, per niente è gradito  
Ora lo ho assodato, è vero, proprio vero

Il vero ho proferito, per dirlo alle persone  
Quelli a cui ho parlato, m'hanno dato afflizione  
Malvagio mi hanno visto, persino più del faraone  
Il vero, or'ho percezione, non son molti che l'amano

La verità ho detto, ai capi della nazione  
Ogni cosa ho spiegato, al cittadino comune  
Su quello che hanno fatto, all'ala d'opposizione  
Ora c'è complicazione, mi fan pagar la verità

Quando il vero ha stretto, come è sua consuetudine  
Loro hanno pensato, meglio pormi in prigione  
Afferrarmi presto presto, e mettermi nel bastione  
Ivi subir punizione, perché mi pentissi di dire il vero



Kweli yanipasha tabu, ndugu yangu niamini  
Na nyingi mno adhabu, za moyoni na mwilini  
Yote haya ni sababu, ya kunena kweli hini  
Ndipo sasa naamini, kweli i utungu kweli

Kweli menibaidisha, na huko kwetu mjini  
Pia menitenganisha, na walo wangu nyumbani  
Kuja kuniadhibisha, kwa kunileta ngomeni  
Yote sababu ni nini? Ni kwamba mesema kweli

Kweli menifunga ndani, ya chumba nde sitoki  
Kutwa kucha ni chumbani, juwa kuota ni dhiki  
Na mlinzi mlangoni, yu papo kattu ha'ndoki  
Nilindwavyo bilhaki, ni kama simba marara

Kweli yanilaza tini, ilo na baridi kali  
Ningawa burangetini, natetema kweli kweli  
Na maumivu mwilini, daima ni yangu hali  
Shauri ya idhilali, ya kulazwa simitini

Kweli japo ni ngomeni, kwenye kuta ndefu nene  
Kabisa sitangamani, na mahabusu wingine  
Na lengo kubwa nadhani, ni: nilonalo 'sinene  
Hazuwa mambo mingine, kwa kuambukiza watu

Kweli pia meninyima, haki zilizo ngomeni  
Wangu kuja nitizama, hilo haliwezekani  
Haya nnayoyasema, ndivyo yalivyo yakini  
Baruwa sitakikani, kwandika wala kwetewa

Sendi mbele 'tasimama, sikupi kwa tafswili

Il ver mi dà difficoltà, fratello mio credi questo  
E castighi in quantità, di corpo e spirito  
Tutto perché la verità, è quel che ho proferito  
Ora l'ho realizzato, il vero brucia invero

Il vero m'ha isolato, rispetto alla città mia  
Inoltre m'ha separato, da casa, dalla famiglia  
Castigare mi ha fatto, portare alla bastiglia  
Perché 'sta condizione mia? Perché ho detto la verità

Il vero m'ha rinchiuso, fuor non esco dalla stanza  
Dall'alba a sera al chiuso, stare al sole è sofferenza  
E la guardia sta fisso, alla porta senza movenza  
Sott'ingiusta sorveglianza, come fossi una tigre

Il vero giacer m'ha fatto, sul freddo pavimento  
Anche se sono coperto, io tremo davvero tanto  
E 'l corpo indolenzito, quest'è sempre il mio stato  
P'esser steso sul cemento, a mo' di umiliazione

Sebbene stia nel fortino, con alti e spessi muri  
Mescolar manc'un pochino, mi posso ai prigionieri  
E 'l fine sia, immagino: che non dica i miei pensieri  
Che io contagi gli altri, provocando altre storie

Il vero m'ha pur privato, dei diritti carcerari  
Mai essere visitato, posso dai miei familiari  
Tutto quello che racconto, è così senza misteri  
Lettere posso ai cari, mai scriver né ricevere

Mi fermo non vado oltre, non sarò più dettagliato

Kusudi nirudi nyuma, kwa ubeti wa awali  
Ili nipate kusema, imani yangu kamili  
Ujuwe kwa jambo hili, mtima wangu ulivyo

Nilipoenua kimo, kutaka niseme kweli  
Nilidhani yaliyomo, hineni sina aili  
Kanama wangu mdomo, waja fungika kauli  
Nisiseme bilkuli, kuwaeleza wanati

Mno wanganiadhibu, adhabu kila namna  
Na mangi yanganiswibu, ya usiku na mtana  
Hayatakuwa sababu, ya kuniasa kunena  
Kweli nitapoiyona, tanena siinyamai

Mateso yao yangawa, nda kuumiza mtima  
Hayatakuwa ni dawa, ya kutonipa kusema  
Ni bure wajisumbuwa, nilipo nnasimama  
Si 'mi wa kurudi nyuma, kweli ilipo 'tasonga

Ama hakika mwendani, kwa mwenye moyo wa sawa  
Mateso ya duniani, wakati kijaaliwa  
Hushukuru Rahamani, kajikaza kutukuwa  
Nami yangawa yakuwa, hikaza moyo si ila

Mateso humbadili, aso na moyo thabiti  
Apawapo idhilali, japo ingawa katiti  
Huona ni afadhali, awate yakwe ya dhati  
Ela langu siiwati, n'shishiyelo ni lilo

Wangi washambuliwa, waneni wa kweli hiyo  
Na wangi washauliwa, kwa kutobadili moyo

Indietro voglio tornare, alla strofa del debutto  
Perché io possa spiegare, qual è il mio credo certo  
Sì che tu sappia con questo, come è il mio animo

Il giorno in cui per dire, il vero mi sono alzato  
Pensavo che'l proferire, non fosse giammai sbagliato  
Son stati lest'a venire, e la bocca m'han tappato  
Affinché non dessi fiato, spiegando ai cittadini

Anche se m'han punito, con pene su ogni fronte  
E molte cose ho subito, sia di giorno che di notte  
Non sarà il modo questo, per non farmi dire niente  
Se del vero son vedente, parlerò non starò zitto

Le torture che danno, anche se mal posson fare  
Un rimedio non saranno, per non farmi più parlare  
Il loro tempo sprecano, qui fermo voglio restare  
Io non mi voglio voltare, vado avanti verso 'l vero

O amico certamente, chi ha 'l coraggio del giusto  
Quando la pena è presente, ch'il destino gli ha dato  
E' grato a Dio Clemente, e resiste in quel stato  
Anche io nonostante tutto, provo a farmi coraggio

Le torture di solito, cambian chi n'ha saldo cuore  
Quando viene umiliato, per poco che possa essere  
Ritiene migliore atto, la sua convinzion lasciare  
Ma io non posso lasciare, a questo io m'afferro

Molti hanno attaccato, che il vero avean detto  
Molti hanno ammazzato, perch'idea non han cambiato

Na mimi nimeradhiwa, ku'yandama sera hiyo  
'Tafuwata zao nyayo, n'shishiyelo ni lilo

Atwambizile Rasuli, kipenzi Bwana Mn'gu  
Ya kwamba tuseme kweli, japokuwa i utungu  
Na mimi siibadili, ni yiyo imani yangu  
Nililoamini tangu, ni lilo hilo sil'ati

Kweli naitiya tamma, nikuage ndugu yangu  
Kweli si mwenye kukoma, kuwambiya walimwengu  
Kweli si'yati kusema, katika uhai wangu  
Nami kwa upande wangu, hi'yambiwa 'takubali

*Septemba 1969*

Ed io sono appagato, di accoglier questo fato  
Seguirò l'orme da dietro, a questo io m'afferro

Ci ha detto il Profeta, di Dio Signore l'amato  
Di proferire verità, s'anche dolor ci ha dato  
Ed io mai l'avrò scambiata, è il mio credo senz'altro  
Ciò che ho sempre creduto, è questo e non lo mollo

In verità deo andare, tuo fratello ti saluta  
In verità io di parlare, non posso farla finita  
Verità non vò lasciare, di dire nella mia vita  
E anche io a mia volta, se mi vien detta l'accetto

*Settembre 1969*

## **Tuza moyo**

Akhi tuliza mtima, uwate kusunoneka  
Hakuna lisilokoma, siku 'kifika 'tatoka  
Kusubiri ni lazima, na kumuomba Rabbuka  
Wasiya wako 'meshika

*Novemba 1969*

## **Placa l'animo**

Fratello mio placa'l core, finiscila di soffrire  
Non v'è che non h'a finire, un giorno potrò uscire  
Aspettar è di dovere, e invocar il Signore  
Ho colto 'l tuo ammonire

*Novembre 1969*



## **Kuno Kunena**

Kuno kunena kwa nini, kukanikomeya kuno?  
Kwani kunena kunani, kukashikwa kani vino?  
Kani iso na kiini, na kuninuniya mno  
Kanama nako kunena, kwaonekana ni kuwi

Kana na huku kunena, kunenwa kakutakiwi  
Kuna wanakokuona, kunena kwamba si kuwi  
Kunena wakikuona, kukuita kawakawi  
Kunena kana kwanuka, nikukome kukunena?

*19 Julai 1970*

## Questo parlare

Ma questo parlare perché, mi ha qui imprigionato?  
Perché 'sto parlare com'è, ch'è con rabbia castigato?  
Una rabbia senza perché, che mi ha sì indignato  
Caspita questo parlare, malvagio può apparire

Seppure questo parlare, non lo si può proferire  
Taluni posson pensare, che male non sia il dire  
E sentendo 'sto parlare, venir a interloquire  
Se il mio parlar vi puzza, dovrei smetter di parlare?

*19 luglio 1970*

## 'O pparlà

I' pe pparlà mo stongo ccà nzerrato,  
aggio parlato e m'hanno mazzariato.  
'O nuozzolo r' arraggia m'ha affucato,  
è malommo chi rice 'a verità.

I' nun m'agliuttarraggio maie 'o pparlà:  
è 'o populo ca 'o vvo', che pozzo fa?,  
si me sente parlà arrispunnarrà.  
Chello ca rico puzza e aggi' 'a stà zitto?

*(Mimmo Grasso)*

## **Siwati**

Siwati nshishiyelo, siwati; kwani niwate?  
Siwati ni lilo hilo, ‘talishika kwa vyovyote  
Siwati ni mimi nalo, hapano au popote  
Hadi kaburini sote, mimi nalo tufukiwe

Siwati ngaadhibiwa, adhabu kila mifano  
Siwati ningaambiwa, ‘tapawa kila kinono  
Siwati lililo sawa, silibandui mkono  
Hata ningaumwa meno, mkono siubandui

Siwati si ushindani, mukasema nashindana  
Siwati ifahamuni, sababuye waungwana  
Siwati ndangu imani, niithaminiyo sana  
Na kuiwata naona, itakuwa ni muhali

Siwati nimeradhiwa, kufikwa na kila mawi  
Siwati ningaambiwa, niaminiyo hayawi  
Siwati kisha nikawa, kama nzi; hivyo siwi  
Thamma nakariri siwi, na M’ngu nisaidiya

*15 Machi 1970*

## **Non mollo**

Non mollo ciò che professo, non mollo, v'è presupposti?  
Non mollo è sì lo stesso , l'afferro a tutt'i costi  
Non mollo son io ed esso, qua o in altre parti  
Finché nella tomba tutti, anch'io, sepolti saremo

Non mollo pur se punito, con pene d'ogni guisa  
Non mollo pur se attratto, con ogni grassa promessa  
Non mollo quel ch'è giusto, mai staccherò la presa  
Giammai stacco la presa, anche se preso a morsi.

Non mollo, non vi sfido, come voi affermate  
Non mollo, e il fondo, lo capite brava gente  
Non mollo ciò che credo, che stimo enormemente  
E mollarlo certamente, mai sarà possibile

Non mollo, son abituato, ogni mal su me infierì  
Non mollo s'anche m'han detto, che ciò che credo non è lì  
Non mollo o sarei stato, qual mosca; non son così  
Lo ripeto non son così, e Dio mi è d'aiuto

*15 marzo 1970*

## **Mamba**

Nami nambe, niwe kama waambao  
Niupambe, upendeze wasomao  
Niufumbe, wafumbuwe wawezao

Kuna mamba, mtoni metakabari  
Ajjigamba, na kujiona hodari  
Yuwaamba, kwamba 'taishi dahari

Memughuri, ghururi za kipumbavu  
Afikiri, hataishiwa na nguvu  
Takaburi, hakika ni maangavu

Akumbuke, siku yake ikifika  
Roho yake, ajuwe itamtoka  
Nguvu zake, kikomoche zitafika

Afahamu, mtu hajuwi la kesho  
Hatadumu, angatumiya vitisho  
Maadamu, lenye mwanzo lina mwisho

*23 Machi 1970*

## **Il cocodrillo**

Ch'io parli, sì come i parlatori  
Che l'abbelli, e piaccia ai lettori  
Che lo veli, lo svelin gl'intenditori

Tronfio spunta, un cocodrillo nel rivo  
Ei si vanta, e si considera bravo  
Ei vi conta, ch'in eterno sarà vivo

Lo illude, uno stupido pensiero  
Ei vi crede, che'l vigor'è duraturo  
Ei v'ha fede, arrogante e sicuro

Sia memore, il suo giorno arriverà  
'l suo essere, sappia che s'allontanerà  
Del potere, il termine arriverà

Colga bene, l'omo il domani non sa  
Non rimane, se le minacce userà  
La ragione, è che l'inizio fine ha

*23 marzo 1970*

## **Nakukumbuka**

Mi nawe mbali tungawa, nakukumbuka  
Lau ngekuwa na mbawa, ningaliruka  
Ni muhali hili kuwa, nasikitika

Mi nawe mbali tungawa, muhibu wangu  
Kamwe hayatapunguwa, mapenzi yangu  
Hili kaa ukijuwa, wewe u wangu

Mi nawe mbali tungawa, sitahamili  
Pamoja 'takuja kuwa, sote wawili  
Mwombe uhai Moliwa, na njema hali

*1 Mei 1970*

## **Ti ricordo**

Io e te seppur divisi, t'ho ricordato  
Se sol le ali avessi, sarei in alto  
Impossibile da farsi, son dispiaciuto

Io e te seppur divisi, o amata mia  
Or non diminuirà così, la passione mia  
E tienilo a mente sì, tu sei ancor mia

Io e te seppur divisi, sii paziente  
Un dì saremo assisi, unitamente  
Che non veda gli Elisi, prega 'l Clemente

*1 maggio 1970*



## **N'sharudi**

Si mwingine ni yuyule, wa Ki-mvita kijana  
Mzawa mji wa kale, mtaa Kuze kwa jina  
Huwo ndiwo mzi mle, tipuzi ya langu shina  
Basi n'sharudi tena, alo na lake nanene

Nijile tena nijile, mneni nijile tena  
Zangu tomi zinyemele, zinyemele kwa maana  
Tangu siku n'toshile, hi'leyo ndiyo nanena  
Basi n'sharudi tena, alo na lake nanene

Si kwamba nali nilele, ndipo hawa sikunena  
Wala kwamba n'choshile, hahitajiya kusona  
Wala sikucha sichile, kunena n'taloona  
Basi n'sharudi tena, alo na lake nanene

Maozi yangu mbonile, yatizama na kuona  
Na masikizi vivile, nayasikiziya sana  
Ili kwamba yaningile, yalipita jana  
Basi n'sharudi tena, alo na lake nanene

Sitatongowa tongole, leo niya hiyo sina  
Leo sikukusudile, kungali mapema sana  
Mwanzo n'atani niole, mambo nipate yaona  
Basi n'sharudi tena, alo na lake nanene

*22 Julai 1972*

## **Son tornato**

E' il giovan di Mombasa, è proprio lui nessun altro  
In città vecchia ha casa, lì a Kuze dov'è nato  
La radice è proprio essa, l'origine del mio fusto  
Insomma sono tornato, chi ha da dire lo dica

Son venuto, son venuto, a parlare son venuto  
Le mie pene ho taciuto, a ragione ho taciuto  
Da quando sono uscito, solo oggi ho parlato  
Insomma sono tornato, chi ha da dire lo dica

Non ero addormentato, quando lor non ho parlato  
Né che io fossi spossato, e il dormir anelato  
Né che fossi impaurito, di dire quel ch'ho pensato  
Insomma sono tornato, chi ha da dire lo dica

I miei occhi hanno visto, osservato e visto  
Le orecchie altrettanto, bene hanno ascoltato  
Così ancora m'è dentro, quel che ier è accaduto  
Insomma sono tornato, chi ha da dire lo dica

Non spiegherò ciò ch'ho detto, oggi non n'ho proposito  
Oggi non sono disposto, è ancora troppo presto  
Prim'a veder vò lasciato, che riveda il mio posto  
Insomma sono tornato, chi ha da dire lo dica

*22 luglio 1972*

## **Ukurasa bikira**

Pweke ndimi, na ukurasa bikira  
U mnyemi, naudara hiudara  
Hausemi, wala kutowa ishara!

Mekodowa, mato pasi kupepesa  
Sawa sawa, umenyoka ukurasa  
Umetuwa, japo ningaupapasa

Chamba: “Nena, na mimi nakusikiza  
Au guna, aula ninong’oneza  
Umenuna? Basi ngaa niapiza!”

Haujibu, utadhaniya ni mfu  
Au bubu, tena kiziwi kipofu!  
Wan’adhibu, kwake’ye sifui dafu!

Ha-u-maji, hasema ‘taukamuwa  
Si mkwiji, hasema ‘taufunguwa  
Siliwiji, la kutenda hapumuwa

Mkaidi, ukurasa umedinda!  
Liso budi, ndilo la mtu kutenda  
Nd’o narudi, na mtungi wangu shinda!

## **Pagina vergine**

L'io solo è, con la pagina vergine  
Piace a me, la accerchio senza fine  
Non parla né, a dar segni è incline

T'ho fissata, un ciglio senza battere  
Ben diritta, pagina tu lo sai essere  
Resti quieta, pur se ti sto a toccare

Dico: "Parla, ed io sto ad ascoltare  
O brontola, o meglio puoi sussurrare  
Tal nuvola? Ora mi puoi bestemmiare!"

Resta zitta, si direbbe che è morta  
Oppur muta, cieca e sorda per giunta  
Mi tormenta, non posso averla vinta

N' è bagnata, da dire che la strizzerò  
N' è borsetta, da dire che la aprirò  
N' m'è venuta, azione p'aver respiro

Ostinata, tu pagina sei cocciuta!  
obbligata, la via è azione pronta  
E' la volta, torno, la brocca a metà





**Tungo za E. Kezilahabi na tafsiri yao kwa Kiitaliano**

*ya R. Gaudio*

**Poesie di E. Kezilahabi e traduzioni in italiano**

*di R. Gaudio*

## **Fasihi**

Maneno yangu kumeza tena sasa siwezi.  
Lakini kuonyesha ukweli na kuutafuta  
Nitaendelea: mimi ni kama boga.  
Nimepandwa katikati, bustanini,  
Na kama boga nitatambaa chini  
Zote pande, kuikwea miti ya hekima  
Na yote magugu koo kuyakaba.  
Bila woga, bila nyuma kurudi nitashambulia  
Ya binadamu matendo bado yakihema.

Halafu wakati  
Ujao utafika  
Matunda nitatoa  
Makubwa madogo  
Mazuri mabaya

Wakati utafika watakapokuja wajuzi  
Kwa jembe la wino kunipalia.  
Wala mboga za majani watanichuma.  
Utafika, wa maboga kuwa mikata.  
Machafu na safi yatachotwa  
Na nitaingia mitungi ya kila mji-shamba.  
Watoto mikononi mwao watanichezea.  
Chini wataniangusha na kunipasua.  
Lakini mbegu, mbegu zitabaki.

Mimi ninajua  
Hatari sina  
Wajibu msomaji  
Mjini na shamba  
Vizuri kunichambua.

## Letteratura

Parole mie inghiottire ora di nuovo non posso.  
A mostrare e cercare la verità  
continuerò: sono come la zucca.  
Seminata al centro, nell'orto,  
e come la zucca mi diramerò terra terra  
dappertutto soffocando tutte le erbacce  
rampicandomi sugli alberi della sapienza.  
Né paura né esitazione attaccherò  
dell'uomo le ansimanti azioni.

Poi col tempo  
un tempo arriverà  
darò i miei frutti  
piccoli grandi  
buoni cattivi.

Un tempo verrà quando a sarchiarmi i saggi  
col rastrello d'inchiostro verranno e  
coloro che mangiano la verdura mi strapperanno.  
Un tempo le zucche da vino utilizzate  
l'acqua sporca e pulita per attingere.  
Entrerò giare d'ogni città e campagna.  
Le mani dei bambini giocheranno con me.  
Per terra mi getteranno e mi spaccheranno.  
I semi però, i semi rimarranno.

Lo so non sono  
in pericolo  
compito tuo lettore  
in città e campagna  
nettarmi in profondità.



Halafu utafika ule wakati  
Watumia vikombe dhahabu na glasi  
Pembeni kwa chuki kunitupa,  
Na nitakuwa nyuma ya wakati  
Lakini wakisahau wahenga  
Kata na mboga walitumia  
Msingi wa wao utamaduni  
Watakuwa wameutupa.  
Kumbukeni, kumbukeni, kumbukeni.

Poi arriverà quel tempo  
useranno cristalli e ori  
scaraventato negli angoli  
sarò passato dal tempo.  
Ma se dimenticheranno gli avi  
le zucche da vino attingevano l'acqua  
della cultura loro il fondamento  
avranno gettato.  
Ricordate, ricordate, ricordate.

## **Jinamizi**

Watu weusi na weupe  
Mtumbwini walikuwa wamesimama, wametulia,  
Na fimbo ndefu mikononi mwao,  
Na macho yao wameyakazia majini.  
Samaki ambaye, kupata hewa,  
Aliinua kichwa chake juu ya maji  
Utawala wa chuma ulimtoboa fuvu  
La kichwa na kutuwa matumbwini.  
    Halafu nilifikiria Afrika  
    Na siasa kwa ujumla  
    – Mafuvu!

Lakini mara, mamba, kwa maelfu  
Mtumbwi waliukimbilia kwa fujo,  
Mtumbwi kupasuka wakatatuliwa  
Vipande vipande.  
Halafu samaki wote waliinua  
Vichwa vyao juu ya maji  
Na pamoja wakaimba wimbo wa Uhuru.  
Lakini majitu, ambayo kwa mbali  
Yalisimama yakitazama, yalionyesha  
Kicheko kilichoonekana kutokuwa na maana,  
Na kutingisha vichwa kwa njia ambayo  
Haikueleweka maana.

Kwa wakati huo, kutoka bahari  
La magharibi washairi walikuwa  
Wameanza kuimba juu ya kifo cha wadhalimu  
Na sauti zao zilisikika bara zima.

## **Incubo**

Persone nere e bianche  
in piedi sulla barca, in silenzio,  
tra le mani una canna,  
si muovono veloci sull'acqua i loro occhi.  
Per l'aria, il pesce  
sporse la testa oltre l'acqua  
il regime delle armi gli perforò  
il cranio e lo scaraventò sulla barca.  
Africa quindi pensai  
e politica  
- Teschi!

Ma d'improvviso, a migliaia, coccodrilli  
frenetici puntarono la barca  
sventrarono dilaniarono la barca  
pezzo pezzo.  
Poi tutti i pesci vennero a galla  
per vedere oltre l'acqua  
e cantare la canzone della Libertà.  
Ma i giganti, che da lontano  
s'alzarono a guardare, emisero  
una risata che sembrava senza senso,  
ed scossero la testa loro in un modo  
enigmatico il senso.

In quel tempo, dal mare  
d'occidente i poeti iniziarono  
canto della morte degli oppressori  
le voci loro sull'intero continente.

Lakini, niliogopa meno marefu ya mamba,  
Zaidi ya hayo, majitu, ambayo  
Kutoka mbali, yalisimama yakitazama,  
yakicheka na kutingisha vichwa vyao  
Juu, chini, kushoto, kulia.

Ma, ero terrorizzato dai lunghi denti dei cocodrilli,  
in più, i giganti, continuavano  
da lontano, in piedi ad osservare  
ridendo e scuotendo la testa  
su, giù, sinistra, destra.

## **Fungueni Mlango**

Hewa kunikosa  
Na jasho kunitoka ndani ya chumba  
Kwa upweke  
Ninajiona nimefungiwa.  
Sioni madirisha lakini  
Mlango wa karatasi uko mbele yangu  
Ninaugonga kwa mikono  
Kichwa na mabega  
Mlango unatoa mlio kilio,  
lakini mwanadamu hatanifungulia.

Damu

Damu puani, damu mdomoni,  
Damu kichwani itumikayo kama wino.  
Mikono, kichwa, mabega uchovu.  
Kwa kichwa kama cha mbuni  
Mchangani, tena ninaugonga  
Lakini mwanadamu hatnifungulia.

Ninaona kizunguzungu  
Ninapiga kelele kama  
Ng'ombe machinjioni:  
Fungueni mlango!  
Mlango fungueni!  
Lakini mwanadamu hatanifungulia.

## **Aprite la porta**

Aria mi manca  
e il sudore mi cola all'interno della stanza  
per solitudine  
mi sento rinchiuso.

Non vedo finestre ma  
una porta di carta mi sta davanti  
ci batto con mani  
testa e spalle  
la porta cigola funesta  
ma è terra e sangue l'uomo non m'aprirà.

Sangue  
sangue dal naso, sangue dalla bocca,  
sangue dalla testa usato come inchiostro.  
Mani, testa, spalle spossato.  
Con la testa come di struzzo  
nella sabbia, ancora batto  
ma è terra e sangue l'uomo non m'aprirà.

Estraniato barcollo  
urlo come  
un bue al macello  
aprite la porta!  
la porta aprite!  
ma è terra e sangue l'uomo non m'aprirà.



## **Wimbo wa mlevi**

Kama Mungu angewauliza wanadamu  
Wanataka kuwa nani kabla ya kuzaliwa  
Hilo ndilo lingekuwa swali gumu maishani.  
Na watu wangeishi kujutia uchaguzi wao.  
Mume angejutia hali yake na mke asingetaka kuwa  
mke  
Mtawala na kabwela, mrefu na mfupi  
Mweusi na maji ya kunde, mwembamba na mnene  
Wote wangetamani kuwa kinyume cha walivyo.  
Sijui nani angekuwa nani.  
Lakini mimi mlevi ningependa kuwa ye yote  
Mradi tu niruhusiwe kunywa pombe yangu.

Hapo nyumbani kwa baba Madaka hamjambo!  
Ni usiku mi napita nakwenda zangu!

## La canzone dell'ubriacone

Agli umani prima di nascere, se Dio  
avesse chiesto, chi avrebbero voluto essere  
sarebbe stata la domanda più difficile della vita.  
Col rimorso per la propria scelta avrebbero vissuto.  
Il marito avrebbe rimpianto il suo stato e la moglie  
non avrebbe voluto essere moglie,  
il dominante e il dominato, l'alto e il basso  
pelle nera e bruna, secco e chiatto  
tutti avrebbero voluto essere il loro opposto.  
Non so chi sarebbe chi.  
Io sono un bevitore e sarei chiunque  
gli sia concesso di ubriacarsi.

Qui da Madaka tutto bene?  
È notte, passavo, sto tornando a casa!

## 'O mbriaco

Si 'o Pataterno all'uommene spiasse  
'e cagnà sciorta primma 'e stà ccà nterra,  
chesta rint' 'o ccampà fosse quistione  
tosta e senza risposta, agliommerata.  
'O marito vulesse turnà a fà 'o scaurachiuovo  
e 'a mugliera na zita ca zetiella.  
E po 'o lazzaro e 'o Rre, 'o sso'nto ncoppa,  
'o nniro sospirasse ll'acqua chiara  
addò se spogna 'o gghianco r' 'e fasule,  
e 'o sicco e 'o chiatto, ognuno  
addiventasse 'o gemello cuntrario  
'e chello ca pe tuocco ll'è tuccato.  
Nun saccio cchiù chi fosse chi e cu chi.  
Ma io so' mbriaco e songo tutte quante  
si 'o ppoco 'e birra scenne futo ncanna.  
Se sta ô ccauro, ccà, â casa 'e Razzullo.  
È notte, chi so' stato se sose e se ne va.

*(Mimmo Grasso)*

## **Safari**

Wakati nisafiripo kwenda mawioni usiku  
Nitazichuma karanga zote zing'aazo angani  
Na kuziweka ndani ya mifuko ya suruali langu;  
Kisha nitazila moja moja toka mifuko iliyotuna.  
Nitakapofika nitafungua kinywa kwa chapati  
Ya dhahabu kabla haijapoa kilimani;  
Halafu hapatakuwa na mwanga tena,  
Kwani taswira na sitiari zote za nuru  
Hazikutufikisha pasipo giza.  
Kwa hiyo basi kama mkulima kipofu  
Nitapanda mbegu gizani.

## Il viaggio

Il tempo del mio viaggio verso l'alba la notte  
coglierò tutti i baccelli lucenti in cielo  
e li metterò nel fondo delle mie tasche  
finché piene ad uno ad uno li mangerò.  
Quando arriverò aprirò la bocca per il *chapati*  
d'oro prima che si freddi sulla collina;  
dopo non ci sarà più luce,  
tutte le immagini e le metafore della luce  
non ci hanno condotto dove non c'è oscurità.  
Per questo allora come un contadino cieco  
spargerò semi nell'oscurità.

## **Kuishi**

Asubuhi, wanaume wakaanga mbegu zao,  
na wanawake washangilia “wazo”.  
Nchi gumba, ukunga umekwisha.

Kulikuwa na wakati tulikuwa  
Sasa mcheko wajaza utupu wa  
Pale tulipokuwa. Hatupakumbuki.

Nchi imezeeka haraka na kuchakaa.  
Haikumbuki tena majina ya watoto wake,  
Na watoto hawaitikii tena mwito.

Wazee sasa, twaua chawa kwa kucha.  
Tusemalo halisikiki, isipokuwa  
Kulikuwa na wakati tulikuwa.

Usiku twaota ndoto na kuwika.  
Kama kufikiri kumekwisha  
Kuishi kungaliko?

Mwangwi wa utupu wazomea.  
Asubuhi wasichana wakaanga mbegu zao,  
Na wavulana washangilia “wazo”.

## Vivere

Di mattina, i semi loro gli uomini arrostitiscono  
e l'“idea” le donne accolgono.  
Terra sterile, l'aiuto al parto inutilizzato.

Ci fu un tempo che fummo  
ora il riso riempie il vuoto  
lì dove eravamo. Non lo ricordiamo.

Terra in fretta invecchiata e abusata  
non ricordi più dei tuoi figli i nomi  
e più non rispondono alla chiamata.

Anziani ora, con le unghie uccidiamo pidocchi.  
Inascoltato ciò che diciamo, anche se  
ci fu un tempo che fummo.

Di notte sogniamo e cantiamo.  
Se terminato è il pensare  
persiste il vivere?

L'eco del vuoto fischiano.  
Di mattina, i semi loro le ragazze arrostitiscono  
e l'“idea” i ragazzi accolgono.

## **Wakati Fulani**

Wakati fulani mende huangukia mgongo  
Na hushindwa kujigeuza.  
Sisimizi kishujaa humshambulia  
Hadi kwa zake juhudi, hujigeuza mbio.  
Ashindwapo hunyonywa uta  
Na mabaki kusombwa shimoni  
Hadi kifupa cha mwisho.  
Wakati fulani usojulikana  
Wakati fulani usotegemewa.  
Binadamu huangukia mgongo.

Wakati fulani nyota hukonyeza  
Binadamu  
Hupanda mti  
Huko juu hutamba nyimbo  
Hadi ghafla wakati fulani  
Usojulikana wala kutegemewa  
Vichaa viziwi hukata mti shinani.

Wakati fulani twasubiri kuche  
Kama mtoto mdogo aliyesikia  
Embe bivu zito likidondoka usiku.  
Wakati fulani twamsaka paa gizani,  
Wakati fulani twataka kumshika mbogo,  
Wakati fulani kwa machozi twatamani  
Tusichonacho na kuwa tusicho.  
Wakati fulani twakurupuka  
Kama buibui aliyehisi  
Mtegowe unatingishika.

## Un certo tempo

Un tempo ciclico cadere sulla schiena  
di una blatta e non riuscir a girarsi.  
Attaccare ciclico coraggioso  
con tutta l'energia delle formiche, girarsi velocemente.  
Perdendo inarcato essere svuotato dentro  
e i resti nel formicaio trasportare  
fin all'ultimo ossicino.  
Un tempo non è dato sapere  
un tempo non è atteso  
dell'umano arriverà ciclico cadere sulla schiena.

Un tempo ciclico occhiolino delle stelle  
all'umano  
sull'albero s'arrampica.  
Lì su narrare canzoni  
finché all'improvviso un tempo  
non è dato conoscere né attendere  
il tagliare ciclico dei pazzi sordi dell'albero.

Un tempo aspettiamo l'alba  
come un bimbo che ha sentito  
un mango maturo e pesante cadere di notte.  
Un tempo cacciamo la gazzella nell'oscurità.  
Un tempo stiamo per afferrare il bufalo,  
un tempo struggentemente aneliamo  
Ciò che non abbiamo e che non siamo.  
Un tempo ci precipitiamo  
come un ragno che percepisce  
la sua trappola vibrante.



Kujua na kutojua wakati,  
kutegemea na kutotegemea  
twaishi kwa kujikongoja  
tukisema kimoyomoyo  
kwa akili sinzinzi  
wakati fulani utafika,  
hadi wakati wawa kifo.  
Kutojua ni kujua.  
Kuishi ni kufa.

Il sapere e non sapere il tempo,  
dipendere e non dipendere  
viviamo trascinandoci  
dicendo in cuor nostro  
con la testa sognante  
arriverà un tempo,  
finché il tempo sia morte.  
Non sapere è sapere.  
Vivere è morire.

## Wimbo wa Unyago

Ishi kijana ishi, ishi maisha yako  
Wazee waliishi yao  
Sasa yamebaki kwako.  
Ukabila ni utumwa  
Olewa msichana olewa  
Olewa chaguo lako  
Hiari ni haki asilia  
Achaguaye embe bichi  
Ajua lini litaiva.

Chunga lugha ya ulaghai:  
Usikubali kuitwa kipenzi  
Hiyo ki ni ki ya kitoto;  
Asifuye macho yako  
Ataka kuyafumba;  
Asifuye miguu yako  
Ataka usitembee;  
Asifuye meno yako  
Ataka ucheke kijinga.

Akuandikaye barua ndefu  
Ashindwa kusema ukweli;  
Na kadi maneno ya wengine.  
Akupigiae simu kila siku  
Hana la kusema bali haloo:  
Asemaye mumeo hafai  
Nyumbani kwake pia hafai  
Mbwa aliwekwa utumwani  
Kwa kifupa kiso mnofu.

## Canzone dell'Unyago

Vivi giovane vivi, vivi la vita tua.  
Gli anziani vissero la loro  
adesso resta a te.  
Tribalismo è schiavitù  
sposati ragazza sposati  
sposa la tua scelta  
diritto naturale è la volontà  
chi sceglie un mango acerbo  
sa quando maturerà.

Bada ad una lingua fraudolenta:  
non accettare d'esser chiamata amorino  
questo ino è di bambinino;  
chi loda gli occhi tuoi  
vuole che li chiuda;  
chi loda le gambe tue  
vuole che stia ferma;  
chi loda i denti tuoi,  
vuole che come una scema rida.

Chi ti scrive una lettera lunga  
non riesce a dire la verità;  
è un gioco con parole d'altri.  
Chi ti chiama tutti i giorni  
non ha altro da dirti che pronto:  
chi dice che tuo marito non è adatto  
a casa sua anche non è adatto  
il cane messo in cattività  
con un ossicino senza carne.

Ee mama mwenye rutuba  
Zaa, zaa kwa mpangilio,  
Si kufyatua matofali.  
Zaa ukichunga afya yako.  
Tawi lenye matunda mengi  
Huvunjwa na upepo wa tufani.  
Kumbuka  
Kuku aliwekwa utumwani  
Kwa wingi wa vifaranga vyake  
Akashindwa kujenga kiota.

Eh signora feconda  
genera, genera con progetto  
non per sfornare mattoni.  
Genera secondo la tua salute.  
Il ramo con molti frutti  
è rotto dal vento del tifone.  
Ricorda  
la gallina messa in cattività  
per molti dei suoi pulcini  
non può costruire un nido.

## **Dikteta**

Kama wajiona ni wewe pekee  
Uwezaye kufikiri  
Ulikufa karne nyingi zilizopita.  
Kilichobaki ni wako mweweseko.  
Wale uliowakemea, uliowaweka ndani  
Uliowadhulumu na uliowaua  
Mawazo yao sasa milizamu  
Ambamo watoto hucheza kwa furaha  
Na kunawa shombo uliloliacha.

Madaraka ni ndoto isiyotegemewa.  
Ni kuvaa kofia juu ya gari wazi  
Lendalo mbio kuvuka mto wa haki  
Ambao daraja lake limechukuliwa  
Na mafuriko ya sheria ulizovunja,  
Ambalo breki zake ni roho za watu  
Na matairi yake ni mafuvu manne  
Ya wale uliowaita vichwangumu  
Haini namba wani wa fikra zako.

## Il dittatore

Se credi d'esser il solo  
a saper pensare  
sei morto diversi secoli fa.  
ciò che resta è il tuo farneticare.  
Coloro che hai denigrato e rinchiuso  
che hai represso e ucciso  
acqua zampillante le loro idee  
dove i bimbi che giocano felici  
e lavano la puzza di pesce da te lasciata.

L'autorità è inaspettato sogno.  
È attraversare il fiume dei diritti  
spazzato via il ponte dal diluvio delle leggi che hai violato  
sfrecciando su una cabrio con in testa un cappello  
i suoi freni degli uomini le anime  
le sue ruote quattro teschi  
di chi hai chiamato testadura  
il tradimento number uàn dei tuoi pensieri.



## **Kirudi kina shaka, shuku na kero**

Kirudi ni zaidi ya tabia.  
Tupa jongoo na mti wake nje ya nyumba  
Katika dimbwi la sahai.  
Huko katika kimya atajinyoosha  
Na kisha kutembea akipapasa kila kikwazo  
Akipindapinda kwa imani kunjufu  
Kuwa anakwenda mbele.  
Asubuhi utamkuta tena ugani  
Akitafuta pa kupenyeza  
Kwa shuku utamtupa tena mbali nje ya ua.  
Jioni utamwona akizunguka nyumba  
Na miguu zaidi ya mia.

Wapo pia kunguni, chawa na viroboto.  
Walisema “kikulacho ki nguoni mwako”  
Utafua nguo zote kwa maji moto  
Na kuzinyoosha kwa moto mkali  
Nyoa kipara na nywele motoni tupa.  
Bado kuna uhai ndani ya pindo.

Tumbua majipu yaliyo kwapani  
Si muda yatahamia pasipo semeka.  
Yabidi kuondoa aibu na huruma moyoni  
Na kuitwa katili.  
Kirudi ngángánizi dawa yake “kweli”  
Fumua mfumo mzima  
Ondoa mapindo na mafundo.

## **Dubbio, sospetto e tormento nel ritorno**

Ritornare è più che un'abitudine.  
Getta millepiedi e l' albero fuori casa  
nella palude della dimenticanza.  
Lì dov'è silenzio si stiracchia  
e poi camminando accarezza ogni ostacolo  
serpeggiando sicuro e contento  
del suo andare avanti.  
Di mattina lo ritrovi in aperto campo  
in cerca di una fessura  
con sospetto lo butterai fuori dal circondario.  
Di sera lo vedrai circondare casa  
con cento piedi.

Ecco cimici, pidocchi e pulci.  
Dicono "ciò che ti mangia lo indossi"  
laverai tutti i vestiti con acqua bollente  
e con ferro rovente li stirerai  
radi capelli e peli buttali nel fuoco.  
C'è ancora vita nell' orlo.

Riconosci gli ascessi sotto le ascelle  
tra non molto si trasferiranno dove non si dice.  
Devi allontanare vergogna e compassione dal cuore  
e invocare lo sterminio.  
Ritornare caparbio è la "vera" soluzione  
Sciogli l'intero ordito  
disfa orli e le cuciture tutte.

Nyota zinazoashiria kilimo na mavuno  
Zimezibwa na wingu zito.  
Hakuna kirudi angamizi  
Kikeracho kama rushwa iliyokithiri.

Le stelle segno di coltura e raccolto  
sono sottratte da una greve nuvola.  
Non c'è ritornare annichilente  
ciò che tormenta come dilagante corruzione.





*Prodotto da*

**IL TORCOLIERE** • *Officine Grafico-Editoriali d'Ateneo*  
UNIVERSITÀ DEGLI STUDI DI NAPOLI "L'Orientale"  
finito di stampare nel mese di Aprile 2017







